**OORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| **Ndugu Yahya Khamis Hamad** | **Katibu wa Baraza la Wawakilishi** |

**Kikao cha Saba – Tarehe 25 Mei, 2015**

*(Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Mwenyekiti (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa mwaka 2015/16. Naomba kuwasilisha**.**

**Mhe. Abdalla Juma Abdalla (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala):** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuweka mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa mwaka 2015/16. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

**MASWALI NA MAJIBU**

**Nam. 3**

**Mchango wa zao la Mpira katika uchumi wa Zanzibar**

**Mhe Ali Salum Haji (Kny Mhe. Shadya Mohammed Suleiman): -** Aliuliza**:-**

Mhe. Mwenyekiti kabla sijauliza swali kwa niaba ya Mhe. Shadya Mohammed Suleiman napenda nitoe pole kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa msiba alioupata kwa kufiwa na dada yake baba mmoja mama mmoja. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi amin.

Baada ya hilo naomba sasa kwa niaba ya Mhe. Shadya Mohammed Suleiman swali lake namba 3 lipate majibu.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Pili ilianzisha kilimo cha miti ya mipira ili kusaidia uchumi wa Zanzibar. Naiomba Serikali inieleze ni kwa kiwango gani zao lile linasaidia uchumi wa Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Fedha -** Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba sasa kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 3 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu ya pili ilianzisha kilimo cha miti ya mpira kama ni moja ya mikakati yake ya kukuza uchumi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha zao la miti ya mpira katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Kwa ujumla maeneo yote hayo yana ukubwa wa hekta 1,262.

Mhe. Mwenyekiti, zao la mpira ni miongoni mwa mazao ya biashara ambayo kwa ujumla wake yanachangia sana katika uchumi wa Zanzibar. Jumla ya tani 1,034 za mpira zimezalishwa kutoka mwaka 2012 hadi 2014 zenye thamani ya TZS. 2,713 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya fedha zilizopatikana kutokana na mauzo hayo ya mpira, pia wastani wa wafanyakazi wazawa 400 wamekuwa wakifanya kazi katika mashamba hayo na kulipwa wastani wa mishahahra ya TZS. 690 milioni kwa mwaka na mchango wa *ZSSF* wa TZS. 45.6 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya mapato hayo pia kodi mbali mbali kama vile kodi ya mapato *PAYE*, kodi ya shamba, kodi ya mashirika (*Corporate Tax)* na kodi ya mfuko maalum wa elimu *SDL* pia zimekuwa zikilipwa kama mapato ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla, kilimo cha miti ya mpira kimeweza kusaidia sana kukuza uchumi wa Zanzibar na ustawi wa wananchi wa Zanzibar.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wakati Mhe. Waziri anajibu swali lake amesema kwamba zao la mpira limeweza kukuza mapato ya nchi yetu na kusaidia ajira kwa watu mbali mbali, na kwa kuwa sasa hivi tuna maeneo mengi katika nchi yetu ya Zanzibar hajayalimwa, je, wizara ina mikakati gani ya kukuza kilimo hichi katika maeneo mengine ambayo hayana kilimo cha kawaida.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka mimwambie tu kwamba miti mingi ya mipira kwa sasa imeshazeeka. Mkakati wa serikali pamoja na wale waliokabidhiwa kuendesha miti hiyo ni kuangalia utaratibu wa kuanza kupandisha miti mipya ambayo itakuwa inatoa zao la mpira kwa wingi zaidi. Lakini kama ulivyoeleza mimi nadhani swali lako ushauri wako niuchukue niupeleke Wizara ya Kilimo kama wataona ni muafaka katika maeneo ya wazi au

maeneo ambayo hayajapandwa mazao waweze kupanda miti ya mipira, na kama mpira unakubali katika maeneo hayo basi wao watakuwa na wakati muafaka wa kuweza kuona kwamba jinsi gani ya watakavyoweza kuyaendeleza mazao ya mpira katika maeneo hayo.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Mhe. Waziri kakiri kuwa mipira inaongeza pato la nchi kwa Zanzibar inayozalisha na kuuza nchi za nje. Lakini kwa sababu sisi tunazalisha tu mipira tunaitengeneza na kupeleka nchi za nje, ambako huko inatengenezewa vifaa mbali mbali ambavyo sisi tunavinunua.

Je, kwa kiwango cha mpira tunachozalisha haiwezekani na sisi hapa Zanzibar kuwa na kiwanda ambacho baada ya mpira wetu kupeleka nje kwa matengenezo ya mambo kadhaa ambayo tunayanunua kuyaingiza tena katika nchi tutatengeneza sisi wenyewe na kuuza nchi za nje, ili kuongeza kipato zaidi katika nchi hii.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, wazo la kuwa na kiwanda cha ku-*process* tukaweza kupata *product* za mipira ni wazo zuri. Lakini kwa kiwango cha mpira tunachozalisha kuwa kiwanda kwa sasa kiwanda kile kitakuwa kwa muda mrefu hakifanyi kazi. Kwa hivyo, tuzalishe mpira kwa wingi, tupandishe mipira kwa wingi, lakini wazo la kuwa na kiwanda ni wazo moja safi sana na ni zuri sana.

**Nam. 10**

**Usumbufu wa Usafiri wa Baharini wakati wa kutoka Pemba – Unguja**

**Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny Mhe. Saleh Nassor Juma)** Aliuliza**:-**

Zanzibar imekuwa ikitegemea zaidi usafiri wa baharini kupitia meli za Serikali na zile za Kampuni za watu binafsi. Hii ni kutokana na kuwa ndio usafiri pekee kwa watu wa aina zote kwa maana ya hata wale wenye kipato cha chini. Kwa kuwa meli zote zisizokuwa za mwendo wa kasi hutumia si zaidi ya masaa sita kutoka Unguja kwenda Pemba, na kinyume chake.

Je, ni sababu gani za msingi zinazosababisha kwa meli hizi kutumia chini ya masaa matano pale wanapotoka Unguja kwenda Pemba, na kutumia zaidi ya masaa sita pale zinapofanya safari kutoka Pemba kwenda Unguja jambo linalopelekea usumbufu mkubwa kwa abiria wake.

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano -** Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 10 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumtoa wasiwasi Mheshimiwa kuwa si kawaida meli zinapotoka Pemba kuja Unguja hutumia muda zaidi kama anavyodai, isipokuwa hali hiyo hutokea baadhi ya nyakati kutokana na sababu zifuatazo:-

1. Kama tunavyoelewa kwamba Zanzibar tunakabiliwa na miongo miwili mikubwa ya upepo kwa mwaka yaani Kaskazi na Kusi. Wakati kaskazi hali ya bahari inakuwa ngumu zaidi kwa chombo kinachotoka Unguja kuelekea Pemba, hii ni kutokana na kuwa chombo kinapingana na upepo na mikondo ya bahari, hali hii hupelekea kushuka kwa mwendo wa chombo.

2. Aidha wakati wa pepo za Kusi hali hugeuka na kuwa ngumu kwa chombo kinachotoka Pemba kuelekea Unguja na kusababisha chombo kuchukua muda zaidi wa safari.

3. Kutokana na ufinyu wa miundombinu hususan ya bandari kutokuwa na nafasi ya kuwezesha vyombo vingi kufunga kwa wakati mmoja, baadhi ya wakati chombo hulazimika kupunguza mwendo hususan kinapotoka Pemba ili kikifika gatini kiweze kufunga moja kwa moja pasi na kulazimika kukaa nangani, ili kuepusha kuwachosha abiria waliosafiri kwa muda mkubwa.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa Fedha 2015/16

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Majadiliano yanaendelea, nina Wajumbe 9 ambao wametaka kuchangia katika hotuba hii na naanza na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa na atafuatia na Mhe. Mohammed Haji Khalid na baadae Mhe. Rufai Said Rufai.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa**:Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa asubuhi hii ya leo kunipa fursa na mimi ya kutoa mchango mdogo sana katika Wizara hii muhimu ya Makamu wa Kwanza wa Rais inayosimamiwa na mwanadada Makini mama Fatma Abdulhabib Fereji.

Mhe. Mwenyekiti, kama mwenzangu alivyotangulia kutoa pole kwa dada wa Rais wetu na mimi naungana naye katika kutoa pole hiyo. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti kama unaweza kutengeneza utaratibu mzuri na sisi tukaweza kushiriki katika maziko hayo, tunaomba utaratibu huo utumike ikibidi ili na sisi tupate fursa ya kuweza kuhudhuria katika maziko hayo, na baadae tukija jioni tuweze kumaliza mambo mengine ambayo yapo kwa mujibu wa taratibu zetu tulizoziunda.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo sasa mimi nakuja moja kwa moja katika eneo zima la tabia ya nchi. Michango yangu leo ni miwili tu, nitazungumzia suala la tabia ya nchi lakini pia nitazungumzia suala la Ukimwi.

Mhe. Mwenyekiti, tokea juzi nilikuwa najaribu kwenda moja kwa moja kwenye baadhi ya misaada na michango ambayo ilikuwa inatolewa katika maeneo mbali mbali kwa ajili ya kusaidia sekta hizi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nimeona kwamba katika suala zima la tabia ya nchi ambapo kwa mara hii washirika wa maendeleo wamepanga kutusaidia milioni mia nne na hamsini. Nikiangalia milioni mia nne na hamsini ambazo wahisani wanatusaidia, lakini katika eneo la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hapa pana ziro. Ina maana mchango wa serikali yetu hauko katika eneo hili.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia eneo hili kama ambavyo Mhe. Waziri alipokuwa amesoma hotuba yake hapa kuna maeneo 148 ambayo kwa sasa yanakabiliwa na tatizo hili la tabia ya nchi. Lakini moja ya eneo hilo Mhe. Mwenyekiti, ni eneo ambalo tunalipigia kelele sana eneo la Kizingo, Kilimani pamoja na maeneo ambayo yameanzia Ngazi mia kule.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitarajia baada ile hatua ya miaka mitatu minne nyuma ya kuzungumzia hali halisi ilivyo katika eneo lile, nilitarajia labda katika maeneo ambayo yangelipewa kipaumbele katika kuhakikisha kwamba ile hali tuliyonayo pale inachukuliwa hatua, nilitarajia kwamba eneo la Kilimani au pale tunapaita Kizingo tungeliweza kuona taarifa za muelekeo wake ambapo tunaweza tukanusuru kutokana na ile hali mbaya inayoendelea pale.

Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli katika eneo lile ziara zilikuwa nyingi za viongozi mbali mbali, na wananchi waliingia tamaa kuona kwamba sasa hivi au halafu eneo lile litakuja kuangaliwa kutokana na hali yake ngumu tuliyonayo.

Kwa upande wetu kama jimbo kupitia katika Mbunge wetu wa Jimbo letu la Kikwajuni tuliweza kubahatika kupata msaada ambao baadae utaratibu wake kidogo ulikuwa una utata tukashindwa kupata ule msaada kwa ajili ya kuendelea na suala lile, lakini hapo hapo tulifarijika kwa kauli zilizotolewa hapa na viongozi mbali mbali juu ya uendelezwaji wa eneo lile.

Mhe. Mwenyekiti, lakini leo nasikitika sana katika bajeti yetu ya mwisho hii tukiwa tunaijadili bajeti hii bila ya kuona muelekeo wa aina yoyote katika kulisaidia eneo lile. Hili jambo ni la kusikitika sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa mara nyengine tena nachukua nafasi hii kuiomba serikali kutokana na hali iliyokuwepo pale katika maeneo ya Kizingo mpaka Ngazi mia; maeneo ambayo watu wengi miongoni mwetu huwa tunatumia maeneo yale kwa ajili ya kwenda kufanya mazoezi. Maeneo yale yameathirika sana katika tatizo hili la tabia ya nchi na hapo nyuma miaka mitatu kabla tulikuwa tunazungumzia suala la kunusuru eneo lile ili lisije kuharibika zaidi na athari ile ikaja ikawakuta wananchi ambao wanakaa karibu na eneo lile. Lakini sasa naona ile nyimbo ya kunusuru eneo lile imenyamazika, sasa sijui kama haikuwa na mdundo mzuri au vipi. Lakini ningeliomba sana katika serikali umefika wakati sasa kuhami maisha ya watu ambao wanakaa katika maeneo yale, ili ile athari isije kuleta maafa katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, maji ya bahari sasa ukiachilia mbali kuingia katika maeneo ya nyumba ndogo ndogo zilizopo pale. Kwa mfano Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na eneo pale la Tume, lakini kwa sasa maji yale yanakuja mpaka majumba ambayo wananchi ya kawaida. Imekuwa hakuna tofauti baina ya baharini na yale maeneo ambayo wananchi wanakaa kikawaida, kutokana na vile viumbe baharini ambavyo mara zote sasa vipo katika maeneo yale.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili yale majumba yenyewe sasa hivi, kule chini yameshakaliwa na maji. Kuna maji ambayo yanakaa katika yale majumba ambayo yanatokana na yale matumizi ya watu wenyewe katika yale majumba. Lakini sasa hivi maji ya bahari pia zaidi yanakuja mpaka maeneo yale, imekuwa maji ya namna mbili Mhe. Mwenyekiti, yanachanganyika kwa wakati mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, ninaiomba sana Serikali kabla hatujaendelea au kabla haijatokezea athari ya maafa kwa majumba yale kuja kuanza kuporomoka wenyewe na kuweza kuleta athari kwa wananchi wetu ambao wanakaa katika majumba yale. Naomba kwa mara nyengine kwa unyenyekevu wa hali ya juu, naiomba Serikali ikaangalie uwezekano wa kuweza kutenga fungu kufanya hatua za dharura ili hali ile tuliyonayo pale na angalau basi itafutiwe utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo lile la Kilimani kuna njia pale ambayo maji ya bahari ilikuwa zamani yanazuilika kutokana na ukuta mkubwa ambao upo pale. Sasa hivi ule ukuta umekufa na zile njia zilizokuwa zimetengenezwa pale nazo vile vile zinapitisha maji kama kawaida. Maji yamekuwa hayana kizuizi. Sikataliani na rehma ya Mwenyezi Mungu katika maneno yake anayozungumza kwamba bahari

inavyokula ardhi, lakini utaratibu wa mlo ule ni mlo mkubwa sana, na unatokana na mazingira ambayo hayajitoshelezi katika kuzuia yale maji kwenye maeneo yale.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kwa sababu eneo lile la Kizingo mimi ninalifananisha na eneo la Kizimkazi kule. Eneo ambalo linahisi kama bahari, karibu itakata barabara pale na wale waliokuwa wanatembea na gari baadhi ya maeneo kule ninaona kama tayari wataingia baharini.Naomba sana kwa unyenyekevu mkubwa suala hili, naomba litazamwe upya na lifanyiwe matayarisho na huduma za dharura ili kunusuru watu wa maeneo ya Kilimani na maeneo mengine 147 yaliyobakia, ili wananchi wetu waweze kuwa salama, wanusurike na hali iweze kuwa nzuri. (*Makofi*)

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, ningeliomba katika mwaka huu huu wa fedha ambao tunaotaka kuupitisha hapa pamoja na kwamba Serikali haikuchangia fungu katika mradi huu wa tabia ya nchi. Katika kufanya hatua za dharura, naomba Serikali iangalie katika mfuko mkuu ili basi kuna baadhi ya yale maeneo yatafutiwe ufumbuzi. Ni jambo la msingi tukaweza kuziba ufa kabla ya kuja kutengeneza ukuta uliokuwa mzima ambao utakuwa umeanguka kwa wakati huo. Naomba sana suala hili lifanyiwe utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo kama nilivyosema mwanzo, leo mchango wangu ni mdogo sana ninakwenda katika sekta ya Ukimwi.

Mhe. Mwenyekiti, eneo la Ukimwi kwa upande wa Zanzibar mimi niseme tu kwamba hatukufanikiwa vizuri sana. Kwa sababu *target* yetu ilikuwa ni kuja kuzitimiza zile ziro tatu. Katika vikao vya nyuma maongezi ambayo yalikuwa yamepita na utaratibu pamoja na mipango ambayo iliyokuwa imepangwa.

Lakini ukiangalia kwa sasa ongezeko la Ukimwi katika visiwa vya Zanzibar linakuwa kwa kasi mno. Sasa Mhe. Mwenyekiti, jamani haya maradhi yanatuondoshea viongozi wetu ambao tunawategemea na wananchi ambao tunawategemea kwamba ndiyo watakaoweza kuja kujenga Taifa la kesho. Sasa kutokana na mtiririko wa maambukizi haya kwamba yanakuja kwa kasi mno.

Mhe.Mwenyekiti, nimeanza kupatwa na hofu na kuona kwamba yale mambo ambayo ilikuwa tumeyatarajia; ule mwelekeo wa kuweza kufikia katika zile ziro tatu, sasa mwelekeo ule unapotea na Ukimwi huu umechukua nafasi kubwa, na sijaona bado juhudi hasa zinazochukuliwa katika kuhakikisha kwamba wale watu ambao wanaohusika na masuala yale ya uambukizaji kutokuambukiza wenzao.

Ninachokiona katika vitabu vyetu hivi, nyingi humu naona ni semina pamoja na vikao tu ambavyo semina hizi na vikao hivi kwa mtizamo wangu itakuwa ni wale

wale watendaji wa juu, lakini huku chini kwa wale watu ambao wana matatizo haya, haya maelekezo hayawafikii.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba tubadilishe mfumo wa kuweza kulishughulikia suala zima la Ukimwi ili tuone basi wale waathirika wa virusi hivi vya Ukimwi wanafuatwa kwa ajili ya kupewa taaluma, na hatimaye kuisaidia nchi yetu kutokuendelea na maambukizi zaidi. Inaonekana Mhe.Mwenyekiti, katika sekta ya kuzuia maambukizi hatukufanikiwa vizuri katika suala zima la Ukimwi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana watu ambao wanashughulikia na masuala haya wakiongozwa na swahibu wangu wa karibu na nimefurahi sana kumuona kwamba yupo hapa, juzi nimeonana naye Dkt. Ali Salum Ali ambaye amekuja kuwasaidia Wazanzibari wenziwe katika kunusuru matatizo haya ya Ukimwi. Sasa atumie ile taaluma yake, kwa sababu mimi ninamjua ni mtu mahiri sana na ni mtu makini sana, atumie uwezo wake alionao kuhakikisha kwamba anasaidiana na viongozi wenzake katika kufanikisha suala zima la kupunguza ili wimbi la mambukizi ya virusi vya Ukimwi kwa watu wengine ambao bado wapo salama kwa upande wetu wa Zanzibar.

La mwisho, Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia ningeliomba sasa Mhe. Waziri atakapokuja hapa anisaidie kunifahamisha utaratibu unaotumika katika kugawa hizi fedha kwa zile *sober houses* ambazo zipo katika maeneo yetu ya Unguja na Pemba. Kwa sababu kuna malalamiko, kuna baadhi ya watu ambao wana *sober houses*, wao hawakufanikiwa kupata huu mgao wa shilingi milioni moja na nusu kama ambavyo taasisi nyengine zimepata.

Sasa atakapokuja Mhe. Waziri Mhe. Mwenyekiti, namuomba anisaidie niweze kujua, na kwa sababu gani pale maeneo ya Kwa Said Sukwa, pale fedha hizi za Ukimwi hazikufika.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, kwa asilimia 90, ninabakisha asilimia 10 niweze kujibiwa masuala yangu haya pamoja na kupata mikakati endelevu ya Serikali juu ya mambo ambayo nimeyachangia.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa fursa hiyo. Ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Mohammed Haji Khalid na baada ya hapo ni Mhe. Rufai Said Rufai baadae atakuja Mhe. Mussa Ali Hassan.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa asubuhi hii na mimi kupata nafasi ya kueleza machache sana kuhusu Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha salama tukaja hapa katika shughuli zetu. Nikupongeze wewe kwa kunipa nafasi hii, nimpongeze halikadhalika Mhe. Waziri na watendaji wake wote waliosaidiana katika kuandaa kitabu hichi cha bajeti ya mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Idara zake nyingi ni zile Idara ambazo zina ulemavu wa aina moja au nyengine. Maana yake ni Idara za matatizo nyingi yake; Tume ya Ukimwi, ni Tume yenye matatizo ya magonjwa, walemavu ndiyo kama walivyo jina lao ni walemavu, madawa ya kulevya kama ilivyo ni masuala ya matatizo. Hivyo Wizara hii imejengwa na taasisi zote ambazo zina matatizo mbali mbali. Kwa hivyo ni Wizara ambayo inahitaji kupewa msukumo na mawasiliano ya hali juu katika kutekeleza kazi zao.

Ni Wizara ambayo inahitaji bajeti yake kwa njia moja au nyengine iweze kutimizwa ili hawa walengwa ambao ndiyo wenye matatizo; matatizo yao yaweze kutatuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimefanya udondozi mdogo kutazama baadhi ya Ofisi za Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Hawa wakiwa ni Wizara mbili ambazo takriban zina hadhi moja. Wote ni wasaidizi wakuu wa Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, nimeitazama Idara ya Faragha ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka huu uliomalizika kwa ufupi iliingiziwa asilimia 35 ya mahitaji ya Idara hii. Ni maingizo madogo mno kwa Idara hii ya Faragha ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais.

Lakini nilipekua ya mwenzake Mhe. Makamu wa Pili wa Rais; sisemi pesa ambazo zimeombwa, pesa zinazoombwa kila Idara ina mtizamo wake wa kuomba pesa. Ninasena kile ambacho wameingiziwa na asilimia iliyoingiziwa. Hii moja ilikuwa ni asilimia 35, hii moja ni asilimia 93, zote hizi ni Ofisi za Faragha za Waheshimiwa Makamu wa Rais. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nimeona hii tofauti ya uingizwaji wa fedha kwa Waheshimiwa hawa wawili katika Ofisi zao hizi mbili zenye mfumo mmoja zote ni Idara za Faragha.

Mhe. Mwenyekiti, halafu nimeitazama Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ya Mhe. Makamu wa Kwanza kinachotarajiwa kuingizwa na kinachopatikana na ile asilimia ambayo imeingizwa ni asilimia 35. Hii Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

Mhe. Mwenyekiti, ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa Idara hiyo hiyo imepata mpaka mwezi wa Machi; zote mbili mpaka Machi mwaka huu wameingiziwa asilimia 73. Kwa hivyo, nilikuwa ninatazama hizi tofauti ningeiomba Serikali kwa baadhi ya Ofisi ya viongozi wa aina hii angalau ule mtiririko uingizwaji wa fedha angalau ulingane kwa sababu ni Ofisi zenye hadhi ya aina moja.

Mhe. Mwenyekiti, nimetazama Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka huu unaomalizika, Idara hii ilikuwa ina miradi miwili ya maendeleo. Mmoja ni mradi wa kujenga Kituo cha Tiba na marekebisho ya tabia kwa watumiaji wa madawa ya kulevya. Fedha iliyoombwa ilikuwa ni shilingi bilioni moja na milioni mia nne, fedha zilizopatikana ilikuwa ni mia mbili na hamsini milioni, sawa na asilimia 18 kama kitabu kilivyoonesha.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, tazama kitu tulichokiidhinisha na kile ambacho Serikali wameingiza. Kwa hivyo, ni kweli hapa Serikali imekusudia kituo hichi kijengwe kwa asilimia 18. Kwa hivyo, ndiyo niliposema Mhe. Mwenyekiti, nikasema Wizara hii ina Idara zenye matatizo na pia kuna matatizo vile vile ya kupatiwa hizo fedha ambazo zinatarajiwa zifanyiwe kazi.

Mhe. Mwenyekiti, mradi wa pili ulikuwa ni mradi wa kujengea uwezo kwa utekelezaji wa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi. Mradi huu ulipangiwa pesa kadhaa lakini zilizoingizwa ni milioni mia mbili na arobaini na tano, laki sita na ishirini elfu. Hizi ni sawa sawa na asilimia 43. Bado ni asilimia ndogo ingawaje siyo ndogo kuliko zile zilizotangulia.

Mhe. Mwenyekiti, ili Wizara hii iweze kufanya kazi na Wizara nyengine za Serikali, kwa kweli lazima fedha zinazoombwa ziweze kupatikana na tena kwa wakati. Vyenginevyo itakuwa tunawalaumu Mawaziri, tunailaumu Wizara husika, kumbe vile kuna yule ambaye anaingiza hizo fedha kwa kima fulani hakutimiza wajibu wake kwa wakati. Kwa hivyo, ningeiomba Serikali ili Serikali iende vizuri na wananchi wetu waache kuilalamikia, iweze kuwaingizia pesa Wizara zinazohusika kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mazingira ni Idara moja muhimu sana na yenye kazi kubwa na ngumu. Ni Idara ambayo inahitaji iwe na wataalamu wazuri wa mazingira, hasa tukitilia maanani kuwa tabia ya nchi kila siku inakuwa inabadilika.

Mabadiliko haya yanaleta athari ya baharini, angani na hata nchi kavu. Kwa hivyo, ili kukabiliana na hayo lazima kuwe na mikakati madhubuti ya kuweza kukabiliana na matatizo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, ukitembea sehemu mbali mbali utaona jinsi bahari inavyofanya kazi yake kuihujumu ardhi. Mwahala ambamo miaka michache iliyopita ilikuwa ni maeneo ya kilimo, leo kule kwetu mashamba imekuwa watoto wanatega samaki wadogo wadogo *whereas* muda mfupi uliopita ilikuwa ni maeneo ya kilimo.

Kwa hivyo bahari inakuja juu kwa kasi kubwa mno. Mwanadamu baadhi ya mambo Mwenyezi Mungu kampa nguvu ya kuweza kuyadhibiti. Yapo mambo tunaweza kuyadhibiti lakini haya hatutaweza kuyadhibiti kwenye kitabu tu, lazima yafanyiwe mikakati, yapatiwe fedha ili Idara husika iweze kukabiliana na matatizo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, maendeleo yetu baadhi ya wakati ndiyo yanayosababisha baadhi ya matatizo yanayotukabili. Kwa mfano, wanadamu tunatakiwa tuishi katika nyumba nzuri na bora, tunahitaji vifaa vya ujenzi. Miongoni mwa vifaa vya ujenzi ni mchanga ambao ni raslimali inayotoka ardhini, mawe na kadhalika.

Katika kupata raslimali hii kwa kima fulani tunachafua mazingira, lakini pia hatuwezi tukasema tusichafue mazingira hivi watu wasijenge. Kwa hivyo, Idara ya Mazingira iweze kuandaa mikakati maalum ya kuwawezesha watu kuendelea na shughuli zao za ujenzi, lakini na athari ya kimazingira isiwe kubwa kama zilivyo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, upo ukataji wa miti kwa kasi sana wa kutumia dhana mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, mwanadamu katumia elimu aliyonayo kujirahisishia shughuli zake za kila siku za maendeleo.

Watu zamani tulio wengi tunatembea zaidi kwa miguu kuliko kutumia vyombo vyengine, tunapata chombo kidogo cha kusaidia baiskeli, utaalamu umeendelea mapikipiki, gari, ndege na kadhalika. Hii ni kurahisisha usafiri wa mwanadamu.

Mhe. Mwenyekiti, wengine wanaokata miti au zamani kwenye visima vya maji vya ndoo tuliweka roda, ili kurahisisha yule mchotaji wa maji atumie nguvu chache kuliko kama ingekuwa hakuna kile chombo. Kwa hivyo, siku zote mwanadamu anatafuta njia rahisi ya kufanya kazi zake.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe umebakiza dakika tano kumalizia.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Mhe. Mwenyekiti, ofisi hii ilikuwa ianze kuchangiwa leo na imalize kesho. Kwa hivyo, tuna siku yetu moja ambayo tumeitangulia. Ningeomba Waheshimiwa Wajumbe wapewe muda wa kutosha, kwa sababu siku yake ya kumaliza sio leo bali ni kesho. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nitazame kidogo kwa hili kwa kuheshimu hiyo kauli yako, niangalie kidogo hizi programu ambazo tumezipanga.

Mhe. Mwenyekiti, tuna programu moja ya udhibiti wa madawa ya kulevya, lakini Mhe. Mwenyekiti programu hii kwa ujumla wake inatumia pesa nyingi sana, lakini fedha nyingi zinakwenda kwenye mipango na utawala kwa hii Tume ya Kitaifa ya Kudhibiti, na ile inayokwenda kwenye programu yenyewe hasa ni fedha kidogo sana, ni milioni 91,064,000, lakini fedha nyingi zinakwenda kwenye utawala. Je, ni kweli programu hii itatekelezeka, ikiwa fedha nyingi zinakwenda kwenye utawala kuliko kutekeleza ile programu yenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, programu ya mazingira na tabia nchi imepangiwa pesa zile tu za wahisani wa maendeleo tunavyowaita. Kama wahisani hawa hawatoingiza hizo fedha zilizotajwa, programu hii itakuwa haifanyiki. Kwa hivyo, sijui hizi programu zetu au programu hii kama wahisani hawakuingiza hicho walichoingiza, programu hii itakuwaje na fedha nyengine ziliopo ni zile ambazo zinakwenda kwenye mipango na utawala.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina hofu kubwa sana kwa mfumo huu utakuwa mbovu zaidi kuliko ule tuliouacha, utakuwa mbaya zaidi kuliko ule tulioukimbia. Kwa sababu programu zilizopangwa fedha nyingi zinakwenda kwenye utawala kuliko kutekeleza ile programu halisi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hofu yangu bajeti ijayo mawaziri tutakuja kuwauliza, hivi sasa wanaingiziwa 35 *and below*, hapo waje kuingiziwa 25 *and below*, sijui programu ikaja kufeli katika mwanzo wake tutaelekea wapi pengine. Kwa sababu kila siku serikali inatafuta njia ya kurahisisha mambo, lakini mara nyengine inafika pahala ule urahisi wao inakuwa ndio ugumu wao.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anielekeze kidogo, pindipo hawa wahisani tunaowaita wa maendeleo, vyovyote tunavyowaita, kama hizi milioni 450 hawakuziingiza programu hii ya mazingira na tabia nchi tutaitekeleza vipi, wakati ambapo pesa nyengine tumezitia kwenye utawala zote. Nadhani dakika zangu tano hazijamalizika.

Mhe. Mwenyekiti,

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mohammed Haji, muda wako umemalizika.

**Mhe. Mohammed Haji Khalid:** Ahsante sana.
**Mhe. Mwenyekiti:** Ulisema utazungumza kidogo, lakini muda wako umekwisha Mheshimiwa.

Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Rufai Said Rufai. Naomba tujali sana muda Waheshimiwa, kwa sababu wachangiaji ni wengi na kila Mjumbe anataka apate fursa. Kwa hivyo, naomba tusirudie rudie yale ambayo yameshasemwa, lakini twende kwenye hoja pia.

Mhe. Rufai Said Rufai karibu na baada ya Mhe. Rufai atafuata Mhe. Mussa Ali Hassan, na baadaye atakuja Mhe. Bikame Yussuf Hamad.

**Mhe. Rufai Said Rufai:** Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru *Allah Subhanahu Wataallah* na kumtakia Rehma Mtume wetu Muhammad (*S.A.W*). Pia, sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwako, asubuhi hii na mimi kunijaalia ukanipa nafasi hii na mimi nikaweza kutoa mchango wangu mdogo, kutokana na hali yangu niliyonayo.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii nzuri kabisa ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, ambayo ipo mezani kwa ajili ya kupatiwa michango mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu nitaanza katika suala zima la mazingira. Mhe. Mwenyekiti, mazingira ni uwanja mpana, kitu mazingira ni neno ambalo limemzunguka mwanadamu katika maisha yake yote, katika utaratibu wake wa kupata maisha na mambo mengine. Kwa hivyo, tukisema neno mazingira ni vyema kujua kuwa ndio mtiririko katika maisha. Kwa hivyo, ni lazima mazingira yetu tuweze kwenda nayo vizuri, ili tuweze kuishi kwa utulivu katika nchi.

Mhe. Mwenyekiti, tumpongeze sana Mhe. Waziri na watendaji wake, kwa jitihada yao wanayoifanya katika kudumisha mazingira hapa Zanzibar. Suala hili Mhe. Mwenyekiti, sio suala la wizara moja, hili ni suala la serikali nzima ili mazingira yetu yaende vizuri, basi ni vyema serikali ikawa kama vile mnyororo wa baiskeli, ukawa umeshikana meno yake haitoi mwanya katika maeneo ya mazingira. Lakini ikisemwa kwamba iachiwe Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais suala hili la mazingira, kwa kweli itakuwa hatutofika pahala. Kwa sababu kila sekta inahitaji kuyasimamia mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuwapongeza ndugu zetu hawa wa Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais, tuliona kwamba hapa Zanzibar tulianza kuyachafua mazingira katika nyanja mojawapo ni suala zima la mifuko ya plastiki.

Kwa kweli ulikuwa unadhania kama hapa Zanzibar kuna viwanda vinavyozalisha hii mifuko ya plastiki. Ukitembea katika majaa yetu basi utaona kweli kwamba mfuko wa plastiki umetumiwa vya kutosha hapa Zanzibar. Lakini serikali ilipoamua na kusema kwamba mifuko hii ni miongoni mwa mifuko inayochafua

mazingira Zanzibar, na serikali yote ikakubali hili, nadhani hali halisi tunaiona, sio suala linalohitaji tochi, ni suala ambalo linaonekana linavyofanyiwa kazi na hali ya Zanzibar ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hii tunashukuru sana, wenzetu hawa kwa kushirikiana na serikali wamepiga mfano, hata wameonesha katika kitabu chao hivi karibuni walifanya ziara mbali mbali, kuna kilo za mifuko karibuni 759 zimekamatwa na kuangamizwa mifuko hii ya plastiki. Kwa hivyo, ni hongera kubwa, ambayo bado ofisi inalihangaikia hili suala kwa mashirikiano na vyombo vya dola, ili kuhakikisha hili suala halirudi katika nchi yetu kama ilivyokuwa hapo mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti mazingira yamechafuka kwa nyanja mbali mbali. Ukija katika ujenzi wa barabara, ili tupate maendeleo ni lazima tutumie ardhi kwa kujenga miundombinu mbali mbali. Ili tuwe na Viwanja vya Ndege basi ni lazima tutatumia ardhi kwa kupata huduma hizo, lakini tunahisi kwamba sheria haisimamiwi wakati tunapoitumia ardhi yetu ambayo ni ndogo, ile sheria tuliyonayo ya mazingira usimamizi wake ni mdogo.

Mhe. Mwenyekiti hivi karibuni Kamati ya *PAC* ilifanya ziara ya mazingira hapa Zanzibar, hasa kule Kisiwani Pemba na tumejionea wenyewe mashimo yaliyochimbwa katika maeneo ya Micheweni. Hapa makampuni hasa ya *MECCO*, walichimba fusi kwa ajili ya utengenezaji wa barabara. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mashimo hayo yamepita kiwango kile kinachotakiwa na serikali yamezidi mara dufu. Sasa hivi yamekuwa ni visima. Kwa hivyo, yamekuwa ni hatari kwa vijana wetu wadogo wadogo na mvua hizi zinazoendelea, mashimo kama yale yakituama maji basi yanaweza kusababisha ajali kwa vijana wetu.

Kwa hivyo, tunapokosa usimamizi, na sisi wenyewe tutakuwa tunashiriki katika kuchafua mazingira yetu.

Pia, Mhe. Mwenyekiti, tuliwahi kutembelea maeneo ya miradi ya watu wanaochimba matofali, huko tulijifaidia vya kutosha sana. Ule mradi wenyewe wanaochimba matofali wanaita ni mradi uokozi, umewaokoa kutoka katika nyumba za miti, sasa wanaishi katika nyumba za matofali, ni hatua moja ya msingi sana iliyochukuliwa. Lakini kuna ukosefu wa usimamizi. Kina kinachotolewa tofali ni kina kirefu na hatima yake yanabakia mashimo, na mashimo yale maji ya chumvi hayako mbali, na baadhi ya maeneo mengine tayari chumvi inaanza kuja juu, hii ni hatari sana Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, wananchi wanapotafuta maisha ni haki yao, lakini usimamizi ni kitu cha msingi Mhe. Mwenyekiti, na mara nyingi unakuja katika miradi yetu mbali

mbali, usimamizi unakuwa haupo, ndio uchafuzi wa mazingira ukawa unaendelea. Kwa hivyo, suala hili Mhe. Mwenyekiti, kama viongozi wale wenye majukumu ya usimamizi katika mazingira yetu, kama hawakuyasimamia basi hatima yake utakuta mazingira yetu tunayachafua haraka sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea, tuliendelea na ziara ile tukaenda katika maeneo ya Vitongoji. Kule Mhe. Mwenyekiti, wananchi wanazalisha matofali, lakini wamejaribu kuunda kamati mbali mbali na kamati hizi tayari wanapanda miti, na baadhi ya maeneo miti tayari ardhi imeshajaa vizuri. Ukifika wewe mwenyewe utafurahi kwamba tayari maeneo yale wananchi wanayajali na kuyaweka katika hali nzuri.

Sasa wananchi wanahitaji kupewa taaluma baadhi ya maeneo mengine, kwa sababu wameunda kamati zao mbali mbali, na wanaishukuru hii ofisi ambayo tunaichangia viongozi wake walifika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais walifika kule, Mhe. Rais alifika kule na wakatakiwa waunde kamati mbali mbali. Lakini baada ya hapo hakuna lolote lililoendelea. Vijana wale wakaachwa solemba na zile kamati walizoziunda kinachoendelea pale ni lawama tu sasa, kwamba nyinyi ndio mmefanya hivi na nyinyi ndio mmefanya hivi. Kwa hivyo, wameachwa solemba kwa kweli.

Mhe. Mwenyekiti, vijana walipokubali kufanya yale, basi waliona ule umuhimu, lakini wanapokosa ule msukumo basi wanavunjika moyo. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ili kuyajali mazingira, basi ni vyema kabisa tuweze kusimamia yale majukumu ambayo tayari vijana tumewabebesha, ili ile hali ya mazingira yetu yaweze kuja kudumu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwenye suala zima la tabia nchi. Mhe. Mwenyekiti, tukitaka tusitake Zanzibar ni waathirika wakubwa wa tabia nchi. Maeneo 148 haya ni maeneo mengi kutokana na nchi yetu ilivyo. Maeneo haya karibu mengi yao yapo kule kisiwani Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, hasa ukiacha Kisiwapanza, lakini ndani ya Jimbo la Tumbe ni miongoni tunaoathirika na tabia nchi, katika pande yote ya Mashariki ya Kaskazini. Maeneo yote hayo ni mengi na hadi hivi sasa wananchi wengi wanakosa kulima vipando vyao, hasa vipando vya mpunga na vilimo vyengine ambavyo vimo kando kando na mabonde, wananchi hawa wanakosa kupata huduma na kuweza kuendeleza maisha yao.

Kwa hivyo, tukitaka tusitake Mhe. Mwenyekiti, tabia nchi hii imetuathiri sana, na wananchi wamejitolea uanzishaji wa upandaji wa miti ya pwani na miti ya juu. Lakini jambo lolote lile linahitaji msukumo, kwa sababu mwananchi athari yeye

sio rahisi kuiona haraka, lakini viongozi ndio wanaoiona athari haraka. Kwa sababu viongozi wanapata taaluma mbali mbali na wanatembea nchi mbali mbali, mwananchi wa kawaida yeye hafahamu hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kule kwetu watu walikuwa wanasema kwamba huwezi kupanda mikandaa, mikandaa anaiotesha Mwenyezi Mungu mwenyewe, mikoko huwezi kupanda kwa sababu Mwenyezi Mungu mwenyewe ndiye anayeotesha ile. Sasa watu wakishakuwa na taaluma hiyo inakuwa ni tatizo, na wanakuwa hawashiriki vizuri katika kuyaondosha yale maeneo ambayo tayari yameshaondoka ile mikoko.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, athari hii kama serikali haitatoka ikaenda katika maeneo haya na kuwapa wananchi taaluma zaidi na zaidi, basi tabia nchi hii itazidi kuendelea kutokana na itikadi za watu zilivyo. Baadhi ya maeneo tumejaribu kutoa taaluma, tumejaribu kuwatumilia wanafunzi wa madrasa, tumejaribu kuwatumilia wanafunzi wa skuli, ili kuondosha na kupunguza suala hili zima la tabia nchi. Lakini na serikali ijitahidi na hilo, ifuatilie katika yale maeneo ambayo athari zake ni kubwa zaidi, kuliko yale maeneo ambayo kidogo wenzetu baadhi ya maeneo yao hayajahatarika sana.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wangu wa Kinowe kwa Mwanambalo hawa mabonde yao wameshayasamehe, haya ni mabonde ambayo wananchi walikuwa wanazalisha mipunga kwa wingi, na ukitoka mpunga walikuwa wanalima kunde kwa wingi, lakini hivi sasa maji ya bahari yamechukua nafasi.

Na hichi ni kilio na hii ni mara ya ngapi sijui miaka mitano nalilia sana, na Mheshimiwa Fatma ni shahidi Wizara yake niliipeleka kwa Mwanambalo tukaenda tukajionea wenyewe kabisa, lakini bado wananchi hawa kilio chao bado Serikali haijakiona, kwa hivyo naiomba sana Serikali iwajali hawa ni wananchi waliopo Zanzibar, na wao wanalipa kodi kama wanavyolipa kodi wengine. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naliomba sana hili Serikali ilitie akilini.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali yangu kama nilivyokwambia mwanzo naomba nimalizie suala zima la UKIMWI. UKIMWI ni tatizo sugu la nchi, UKIMWI unadhoofisha vijana na UKIMWI tokea tulikuwa na 2. sasa hivi umeshapita hatua. Sababu tunaona labda huu UKIMWI labda mtu anapata kuishi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa una dakika tano.

**Mhe.Rufai Said Rufai:** Kwa kutumia haya madawa yaliyopo, na unapopata kutumia hizi dawa hali yako inakuwa nzuri inaridhisha basi ule uzito wake haupewi nafasi kubwa sana, lakini kila kukicha vijana wetu ndio wanapotea, na vijana ndio rasilimali tukitaka kustaafu, vijana ndio rasilimali, na itakuja kufika

kipindi tukitaka vijana kufanya kufanya kazi hapa iwe tuazime au waje wageni kutoka nchi nyengine kuja kufanya kazi hapa Zanzibar kwa sababu vijana wetu wote wameathirika. Na UKIMWI bosi wake anayeongoza ni madawa ya kulevya, kwa sababu mtu anapoondosha akili akawa na akili nyengine anaweza kufanya lolote lile, kwa sababu baba wa maasi ni ulevi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ili tuuweze UKIMWI, basi kwanza ni kupambana na ulevi, tupambane na ulevi ndio tutauweza UKIMWI, lakini kama unaweka ulevi fulani ni halali na ulevi fulani ni haramu, basi hatutofika hatua yoyote Mhe. Mwenyekiti. Ulevi hata ukawa vipi ni haramu, ni haramu tu, na ulevi ndio unaosababisha matatizo yote. Kwa hivyo tukiendelea kwamba watu wanaendelea kupewa leseni za kuuzia ulevi, basi tujue kwamba UKIMWI utakuja juu zaidi, kwa sababu baba ya maasi ni ulevi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kama Serikali iko tayari kuondosha janga hili la UKIMWI, basi ipambane na suala zima la madawa ya kulevya, kinyume na hivyo bado UKIMWI utawaathiri vijana wetu, na utaendelea kuondosha hadhi ya vijana wetu hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache mimi naunga mkono hoja hii mia juu ya mia, na nashukuru sana Ahsante. *(Makofi)*

**Mhe. Mussa Ali Hassan:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu wakati huu tukaweza kuchangia shughuli zetu ambazo tumejipangia pamoja na kumpa pole Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa msiba uliomkuta wa kufiliwa na dada yake.

Kwanza nianze kuchangia ukurasa wa 19 kuhusu mazingira, Mhe. Mwenyekiti, ninazo sehemu nyingi za uchimbaji mchanga pamoja na uchimbaji mawe, iko haja sehemu zote zinazochimbwa madini haya zipewe kipaumbele kukaguliwa kila baada ya muda, ili kuhakikisha sehemu hizi zinazochimbwa michanga na mawe ziko katika hali ya usalama, kwa kuhakikisha kwamba isitokee athari za mafuriko ambazo zinakuwa zinatokea hivi sasa sehemu hizi. Kwa kweli sio sana Wizara hii kuzipitia kila baada ya muda kuzitizama au kufanya uchunguzi kwa usalama wa wananchi, hasa katika mabonde ambayo hayakuruhusiwa, na Serikali na utakuta hivi sasa yamegunduliwa kwamba yanachimbwa bidhaa hizi bila ya ridhaa ya Serikali.

Ukiangalia hivi sasa sehemu za jimbo langu la Koani utakuta sehemu ya Bungi imefunguliwa sehemu ya mchanga, na inahatarisha kituo chetu cha redio kupata mafuriko ama kuanguka kutokana na kwamba wananchi wa pale wanachimba

mchanga sehemu ambazo hazikuruhusiwa, na wala lile bonde halikuruhusiwa na Serikali kufanya masuala haya.

Iko haja ofisi hii kuhakikisha inafanya uchunguzi kwa usalama wa sehemu hizi pamoja na wananchi kuhakikishiwa usalama wao pamoja na sehemu zao na mali zao.

Si hivyo tutakuta kila baada ya muda, iko haja ya kufanya matayarisho mengine ya usalama au majenzi mengine, na utakuta kwamba Serikali inafanya maendeleo mengi kwa ajili ya wananchi, kama hivi sasa Bungi kuweza kupata kituo kile kizuri cha Redio, lakini hivi sasa kiko hatarini kutokana na bonde hilo la mchanga ambalo linachimbwa bila ya kufanyiwa uchunguzi au kulisimamisha au kuliwekea uzio kwa ajili pasichimbwe mchanga.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, nichangie ukurasa wa 21 kuhusu walemavu. Serikali yetu hivi sasa imeweka bajeti kubwa sana kwa ajili ya wazee ambao wataanzia miaka 70 ili kupewa msaada kuhakikisha kwamba hawapati matatizo ya maisha, na kuondolewa usumbufu ambao Serikali imeona iweke bajeti maalum kuhakikisha kuweza kuwachangia wazee hawa katika bajeti ya mwaka 2015/16, kuhakikishiwa kwamba wawe na pesa kuanzia elfu sitini (60,000) huu ni msaada wao.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ingeliweka mchango kama huo kwa watoto wetu na wazee wetu ambao ni walemavu, na ambao hali zao ni ngumu sana na duni kabisa, badala ya kupewa vipandio tu ambavyo vipo kwenye kitabu chako hichi cha Afisi ambacho kimewasaidia, ni afadhali na wao kuweza kupata mchango wa fedha, ili kuhakikisha kwamba walemavu wetu wanapatiwa uchango huu kwa msaada ili kuweza kujikimu katika maisha yao ambayo ni magumu sana.

Utakuta mlemavu bila ya kukuomba wewe mwenyewe unatoa pesa unamsaidia kutokana na ile hali aliyokuwa nayo, na unamkuta anatembea na kibaiskeli kupita njiani ambacho kilitolewa msaada na Serikali, lakini naona ni vizuri Serikali ingelihakikisha kwamba inawahudumia vizuri walemavu wote ambao wako katika hali ngumu, wakaweza kupewa msaada, tukahakikisha nchi yetu haina walemavu ambao wanapita njiani wakawa omba omba kama ilivyo hivi sasa. Kwa kweli Serikali ingelitoa tamko ni kiasi gani ambacho kitawekwa kwenye bajeti kama ilivyoweza kuweka bajeti ya Wazee, na ikatangazwa katika bajeti hii ambayo tunaendelea nayo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na muda ulivyo niweze kuchangia matatizo ya madawa katika ukurasa wa 26. Matatizo ya madawa ya kulevya, hivi sasa kuna vijana wengi ambao wameathirika kwa madawa ya kulevya iko haja Serikali kuhakikisha kwamba inajenga *sober house* kwa ajili ya kusaidia vijana wetu

kupunguza matatizo na kuweka masomo ili kuhakikisha kwamba vijana hawaendelei kuathirika na madawa haya.

Mhe. Mwenyekiti, ipo haja Serikali kuhakikisha kila Mkoa wa Zanzibar na Wilaya zake wamejengewa *sober house* ili kuhakikisha vijana wetu wanapata masomo ili kujua madhara gani wanayoyapata katika matatizo ya madawa wanayovuta, pamoja na wanaojidunga sindano, lakini hivi sasa utakuta *sober house* utakuta ziko katika sehemu za mjini tu, sehemu nyingi za mikoa yetu hivi sasa hazijahakikishiwa kuwa na masomo ya *sober house*, ili vijana kuhakikisha wanajua nini tatizo la madhara makubwa ambayo yanawapata katika madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa katika jimbo langu kumejengwa uzio muda mrefu sana kwa ajili ya *sober house*, lakini hadi leo hapajashughulikiwa chochote, pana uzio tu na tunahakikisha kwamba sijui uzio ule utafikia miaka mingapi ili kuhakikisha kwamba uzio ule unajengwa *Sober house*, kwa ajili ya wananchi wa sehemu nyingi, na ile ilitegemewa iwe sehemu kubwa sana ya kuweza kuhakikisha kwamba vijana wengi wanaoathirika wanapelekwa katika sehemu hizo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanapewa maelekezo makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, iko haja kuweka fedha nyingi sana hivi sasa ili kuhakikisha kwamba mikoa yetu inapata *Sobher House* kwa wakati, ili kuhakikisha na kuharakisha majukumu ya Serikali ili kuhakikisha wananchi wanapata masomo, na kutatua shida hizi ambazo hivi sasa zinashindikana kabisa kuzitanzua, kwa vile wananchi wanaathirika siku hadi siku, na wananchi wenyewe ni vijana ambao ndio ulikuwa tegemeo la Serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nachangia ukurasa namba 28 kuhusu matatizo ya Ukimwi. Matatizo ya Ukimwi hivi sasa yamesahaulika kabisa kwamba ni madhara makubwa sana yaliyoweza kulisumbua Taifa mpaka tukahakikisha kwamba Ukimwi utakuwa hauna dawa, lakini hivi sasa tumepata dawa za kurefusha maisha tu lakini sio dawa kamili za kuondoa Ukimwi.

Kwa hivyo, hivi sasa hatupati sensa ambazo zilikuwa zinatolewa kila baada ya muda kwa kila mkoa au wilaya pamoja na vitongoji, kila kijiji kuna watu wagapi ambao wameshaathirika na maradhi haya ya Ukimwi. Hivi sasa tunachojua ni fedha tu ambazo zimetengwa kwa ajili ya Ukimwi lakini hatujui wagonjwa wangapi ambao wameathirika na wangapi wanapata tiba kwa ajili ya kuhakikisha kwamba maradhi haya yanapungua, lakini badala ya kupungua utakuta hivi ndio yanazidi kuendelea, kwa vile hata Serikali haitangazi chochote kuhusu matatizo ya Ukimwi katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna haja Serikali kufanya kazi ya ziada ama ya makusudi kuhakikisha kupewa *dose* ya Ukimwi kila baada ya muda kusomeshwa katika sehemu zote za nchi yetu, kuanzia maskulini hadi katika vijiji vyetu kuhakikisha kwamba Ukimwi ni janga.

Kutokana na hali ya wakati pamoja na muda wenyewe kwa leo mchango wangu utakuwa ni mdogo sana, ili kutoa vifungu muhimu tu ambavyo ofisi hii ndio inayohusika iweze kuhakikisha kwamba inazifanyia kazi shughuli hizi kwa wakati na isifumbie macho matatizo makubwa ambayo yanatuathiri sana wananchi wote wa nchi hii.

Zaidi ya hayo sina budi kuhakikisha kwamba Mhe. Waziri anayachukua na anayafanyia kazi kwa wakati, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kutujaalia tukaweza kukutana katika ukumbi huu tukiwa na afya njema sote kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, pia niweze kukushukuru wewe kwa kuweza kunipa fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo sana katika Wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze Wizara kwa jitihada zao wanazozichukua katika kuhakikisha kuwa majukumu haya wanayopewa wanayafanyia kazi kwa uzalendo wa hali ya juu, maana si kwa kifedha lakini kwa uzalendo wa nchi yao kuweza kuhakikisha kuwa masuala yote au majukumu yote waliyopewa basi kwa hali yoyote wanaweza kufanikisha.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukurani zangu hizo nianze katika Idara hii ya Mipango Sera na Utafiti. Mhe. Mwenyekiti, Idara hii watu wengi wameshaichangia kutokana na uingizwaji wake wa fedha, lakini mimi nataka niseme kuwa Serikali kwanza itambue kuwa kila Wizara basi Idara hizi wanatakiwa wazipe kipaumbele, kwa sababu ndio Idara ya Mipango, Sera na Utafiti Wizara yoyote ya Serikali kama haikuwezesha Idara hizi basi hatimaye hakuna litakalokuwa. Kwa sababu hawa ndio wafuatialiaji lakini hawa ndio wafanyaji wa tathmini, lakini hawa ndio wanaojua matokezeo yote katika Wizara yao na mipango yao waliyoipanga, sasa leo kufika pahali Wizara kama hii na majukumu kama haya waliyonayo makubwa ya kijamii na ya kiserikali kwa jumla wakaweza kuingiziwa asilimia 35 ya pesa, basi ni kuwa Serikali nayo haijawa tayari kuona kuwa Wizara wanafanya majukumu yake ipasavyo, serikali haijawa tayari. Japokuwa hali ni ngumu, lakini hizi Wizara ni Wizara za kufanyiwa hii

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ndio za kuwezeshwa ili kuweza kufanikisha ile mipango yao wanayoipanga.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii ina majukumu makubwa. Ukiangalia suala la mazingira ni suala la nchi nzima inatakiwa Serikali ipange mipango yake kutokana na mazingira ya nchi nzima, ili iweze kufanikisha na ili isiweze kupatikana matokeo mengine ambayo kuwa si ya lazima, basi lazima Idara ya Sera, Mipango na Utafiti basi waweze kuangaliwa kwa jicho la huruma.

Mhe. Mwenyekiti Serikali iangalie sana hili, kwa sababu nakumbuka bajeti ya Wizara ya Afya wana idara yao ile wanasema kuna maradhi yasiyopewa kipaumbele, lakini kuna maradhi yasiyopewa kipaumbele sasa hivi yale maradhi yanaonekana yanaathiri jamii.

Sasa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa majukumu yake wanayowapa, bado wanaifanya kuwa ni Wizara iliyokuwa isipewe kipaumbele kutokana na shughuli hizi.

Kwa hiyo, tuiyombe serikali Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni wizara ya kuiangalia kutokana na majukumu yake makubwa. Tukidharau hilo basi hatimaye ni kurithi majanga, kurithi mafuruko, ni kurithi moto unaoingia majumbani uliyokuwa hauna hata njia za kupita, yote hayo yatarithi. Sasa lazima tuangalie hawa Idara hii ya Sera na Mipango iwezeshwe ili iweze kufuatilia na hicho ambacho watakifuatilia ina maana ndicho kitakachojenga mustakbali wa nchi yetu, namna gani tuweze kufikia matokeo kwa haraka au namna gani tuweze kujinusuru na majanga ambayo kuwa ni jukumu lao. Pale ikiwa ile pesa wameingiziwa hawakufanya kazi zao, basi wao ni wachangiaji wakubwa wa maafa yatakayotokea.

Mhe. Mwenyekiti, niiyombe sana serikali kuangalia maeneo muhimu ya nchi kuyapa kipa umbele, ingawa yote ni maeneo muhimu lakini kuna mengine yaangaliwe ili yasiweze kuleta athari zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la mazingira. Suala la mazingira ni suala ambalo kwa kiasi fulani linagusa kila maeneo. Ujenzi wa kiholela unaojengwa pia ni suala la mazingira, lakini ukataji wa miti pia nalo ni suala la kuathiri mazingira, lakini hata ujenzi wa barabara zilizokuwa zinajengwa hazina mpango mzuri zinaathiri mazingira, uchimbaji wa vifusi ovyo nao unaathiri mazingira. Sasa yote haya Mhe. Mwenyekiti, lazima serikali iyone kuipa umuhimu wa Ofisi hii kipaumbele nayo ili waweze kushughulikia nchi kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mazingira juzi katika kitabu cha Makamu wa Pili wa Rais alizungumza moja ni ujenzi wa kiholela watu wanaoujenga, kuna watu wanaotoa vibali vya ujenzi. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na wao wanachangia katika suala hili. Kwa sababu wao katika Halmashauri zetu zilizopo wao wana mtu wao katika Ofisi hizi ili kuweza kushughulikia suala zima la mazingira pale wanapochukua vibali vya ujenzi. Kwa hivyo, hili Mhe. Waziri aje anieleze kuwa kama wana watu wao katika Halmashauri ambazo kuwa ndio watu ndio wanaotoa vibali vya ujenzi atwambie watu wao, hao wapo na kama hawapo ni kwa sababu gani, kwa sababu ni moja kati ya suala la uhifadhi wa mazingira. Mtu asipewe kibali cha kujenga bila ya kujulikana wapi anakwenda kujenga.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine katika mazingira, nimuombe Mhe. Waziri, kuna vikundi vya ushirika watu wanaojitolea katika kuhifadhi mazingira katika upandaji wa miti. Na hawa pia Mhe. Waziri, uwaone watu hawa kuwa ni muhimu na watasaidia serikali yao na wamejitolea kwa nia safi dhidi ya kwamba wamefanya kibiashara, lakini pia na kuhifadhi mazingira yatasaidia. Sasa hivi kuna maeneo mengine baadhi ya mvua hazifiki kutokana na ukataji wa miti unaoshamiri. Kwa hiyo, na hivi vikundi navyo pia basi muweze kuvifuatilia na kuvipa hamasa ili waweze kuendelea na wenziwao basi waweze kufuata hayo mambo mema.

Mhe. Mwenyekiti, niingie kwenye suala zima la dawa za kulevya. Dawa za kulevya nalo limekuwa ni tatizo kiasi fulani, lakini na hilo nathubutu kusema kuwa pia serikali bado haijataka kikamilifu suala hili la kuondoa madawa ya kulevya au kupunguza kwa kiasi fulani dawa za kulevya. Kwa sababu ya kusema hivyo siku zote tunapiga kelele hapa kuwa Zanzibar ni visiwa ambavyo kuwa vimezunguungwa na bahari. Lakini sasa visiwa hivi vinabandari ndogo ndogo ambazo kuwa vyombo vinaingia kutoka nchi nyengine kuingia kisiwa chengine. Sasa hii bado serikali mule hawajawa na udhibiti wa ulinzi nani anaingia na nani anaingia na nini, yeye mtu ataonekana anarudi Kenya anaingia pale Bandari ya Tume hajulikani anachokishusha pale ni kitu gani.

Lakini kusema kuwa serikali haijawa tayari, Mheshimiwa, tulishuhudia hapa sote kulikuwa kunatatizo la magendo ya karafuu, lakini kwa kiasi fulani serikali ilipoona kuwa karafuu hawazipati, basi wakaimarisha ulinzi na kweli walifanikiwa na kuongeza kwao kwa bei, lakini na ulinzi ukashamiri, hili suala likafanikiwa kwa kiasi fulani. Sasa leo kama tunapiga kelele dawa za kulevya na vibandari hivi vinavyojaa, wala hakuna ulinzi, wala hakuna mtu anaeulizwa unatoka wapi au umeingia nini, basi hii itakuwa ni nyimbo ya dawa za kulevya, dawa za kulevya. Vyenginevyo, itakuwa ni hatufanikiwi, watoto wetu wataathirika kiasi fulani, wataanza kuvuta sigireti baadae watakula na huo unga.

Serikali hili hawajawa tayari kwa hilo, walipoona pesa hawaipati kwa karafuu walifanya juhudi kwa wakaweka walinzi, basi wamefanikiwa kwa kiasi fulani. Lakini suala hili la kuwa vyombo vinaingia katika bandari hizi ndogo ndogo, wao hata hawashughuliki. Tumeshashuhudia hapa kupitishwa silaha ambazo kuwa zimekamatwa bandari ya Mkokotoni, sijui bandari ya wapi. Lakini sasa tukiendelea kusema madawa ya kulevya yanaongezeka watoto wanaharibika na hali ya kuwa hatujui nini cha kufanya, basi hii itakuwa siku zote ni nyimbo.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine niseme kwamba naipongeza Tume ya Ukimwi na wao juu ya michakato yao wanayoifanya. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi Ukimwi umekuwa kama mtu anaogopa maradhi ya sukari na *pressure* sasa hivi, lakini Ukimwi kwa serikali wanavyohamasisha na kuweza kuwahifadhi hawa na kutaka wapatiwe haki zao, kwa hivyo, naona kwa kiasi fulani watu wamepungua hofu na huo mchezo unachezwa wala hawana matatizo. Kwa hiyo, tumshukuru Mwenyezi Mungu na kila mmoja atabeba mzigo wake yeye mwenyewe. Kwa hivyo, suala hili nashukuru suala kuwa watu wameondoa hofu, wanakufa kwa *pressure* na sukari na mambo mengine ni wengi kuliko wanaokufa kwa Ukimwi, zote hizi ni juhudi za serikali, kwa hiyo, tuendelee nayo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini suala jengine nimpongeze Mhe. Waziri, katika kiambatanisho chake hichi, kuna aina za idadi za walemavu. Niwapongeze na niwashukuru kwa kuona kuwa watu wenye ulemavu na wao wanajaliwa kama ni jamii na wao wana haki ya kuweza kufuatiliwa kutokana na zile shida zao ambazo ni za kimaumbile ambazo kuwa Mwenyezi Mungu amewajaalia.

Hapa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, kaandika "wilaya zilizopewa visaidizi hivi jumla ya watu waliopewa". Lakini sasa nataka anisaidie jambo moja kwa sababu kuna maeneo mengine naona kuna ziro ziro katika hichi kiambatanisho. Je, huku ni kuwa hawapo hao watu wenye ulemavu, kwa sababu visaidizi vimeandikwa lakini huku mbele kuna ziro, hili ningeomba Mhe. Waziri akija anisaidie.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kama nilivyosema mwanzo kuhusu suala la mazingira. Mhe. Waziri katika kiambatanisho chake hichi ametuonesha miradi mbali mbali ambayo kuwa wameifanyia tathmini ya kimazingira kupewa vyeti vya mazingira. Ndio lile suala la mwanzo nililolizungumza. Hii tayari inajulikana kuwa hii ni miradi iliyokuwa ni ya wawezeshaji. Lakini lile suala langu nililolizungumza mwanzo, je, Mhe. Waziri, unatafuta mazingira katika miradi hii tu kwenye maeneo ya ujenzi wa majumba hakuna tathmini mnazozifanya. Hebu Mhe. Waziri, njoo utueleze ni sababu gani za msingi ambazo kuwa nyiye hamna tathmini za kimazingira katika ujenzi holela ambao kuwa siku zote unashamiri katika kisiwa hichi cha Zanzibar na kupelekea tukapata maafa mengi na majanga mengi ambayo kuwa hatukuyatarijia.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Bikame una dakika tano za kumalizia.

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, hizo dakika tano nataka nikuachie wewe mwenyewe utafute mtu mwengine umpe. Nashukuru sana na naunga mkono bajeti hii kwa asilimi mia. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

**Mhe. Ashura Sharif Ali:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa Rehema, aliyetujaalia uhai, lakini pia akatupa na uzima na akatuwezesha kuwepo kwetu hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya wananchi wa Taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, pia, nikushukuru na wewe kwa kunipatia na mimi fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo katika bajeti iliyokuwepo mezani ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuwasilishaji wake mzuri, ameiwasilisha vizuri sana na anastahiki sifa Mheshimiwa huyu mwana mama. Lakini pia niwapongeze watendaji wake Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na wafanyakazi wa Ofisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kusema kwamba wizara hii ina mambo mtambuka yanayogusa kila aina ya mguso wa taasisi nyengine za serikali. Utekelezaji wake unahitaji mashirikiano ya kutosha ili iweze kufikia ufanisi wa kweli. Niseme kwamba Zanzibar tumekuwa na sheria nyingi na hata nyengine inafika mahala tunaanza kuzisahau na kuanza kusema tutunge labda sheria nyengine, tunahisi kwamba zile nyengine labda zimesahaulika. Tumakuwa na maradhi na maradhi haya ni usimamizi wa sheria. Maradhi ya usimamizi wa sheria imekuwa ni tatizo kubwa la serikali yetu. Hili ndilo ambalo linatuathiri katika mambo mbali mbali, nasema kwamba "Tusipoziba ufa, tutajenga ukuta" huo ni utangulizi wangu wa kwanza katika mchango wangu.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye mabadiliko ya tabianchi. Mabonde mengi ambayo wananchi wetu wakiyatumia kwa ajili ya kulima au kilimo kwa upande wa Pemba kwa wakati huu na serikali inasema kwamba "Kilimo ndio uti wa mgongo wa Taifa letu". leo tunajua kwamba Wazanzibari chakula chetu kikubwa ni wali na mabonde ambayo yamevamiwa na maji ni yale ambayo yanalimwa mpunga ambapo wananchi wanajipatia riziki hiyo, wale wasio na fedha za kununua huwa wanalima katika mabonde haya na kujipatia riziki zao au milo yao na bila ya kwenda madukani kwa sababu hawana fedha hizo.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona humu katika kitabu hichi kwamba kuna mambo, mradi maalum nimeona humu. Lakini nikawa nina wasi wasi kidogo, nikawa nataka

nimtazame Waziri wa Fedha kwamba yupo humu ndani? Naona simuoni machoni mwangu, ametoka. Nasema hili nikiwa nina maana kwamba, kuna mpango mpya huu wa *programme basic budget* tunakubali. Ni mpango mzuri unaokubali lakini mpango huu unakubalika na kutekelezeka pale ambapo fedha zake zitatolewa zote ili tuweze kuona hayo matokeo.

Lakini, bajeti tuliyotoka nao nyuma ya taasisi hii ambayo imeweka miradi mbali mbali humu ya maendeleo fedha yake ni ya wahisani tu, kama hawakutoa maana yake hakuna mambo. Kama Shekhe Omar Yussuf serikali haikufanya hilo maana yake haya mambo hayatotekelezeka. Hii mipango yote ililiyopangwa humu ya *PBB* utekelezaji wake maana yake tunauziwa mbuzi au punda kwa mlio, ndio maana ya bajeti hii. Tunaidhinisha sisi hiyo mipango yenyewe bado kutekelezwa, tunaziidhinisha fedha na hatimaye hiyo mipango tutakuja kuona huko mbele matokeo. Kwa hivyo, tayari sisi tunauziwa mbuzi kwa mlio, hatujamuona huyo ng'ombe ila ni kwa mlio tu.

Mhe. Mwenyekiti, wakati huo huo inatueleza wazi namna ya bajeti ya fedha zilivyokuwa zikiingizwa hazikufikia hata nusu kwa kila taasisi, zina asilimia ndogo. Mhe. Waziri wa Fedha, nilitarajia atakuwemo humu ndani ya Ukumbi huu anambiye kwamba ana utaratibu gani wa kuona haya mabadiliko ya tabianchi ambayo maji ya chumvi yamevamia mashamba ya wakulima ambao kwa wakati huu wanashindwa kufanya shughuli zao na wana mradi maalum. Je, fedha hizo Mhe. Waziri, zinaweza kupatikana kwa wakati na wananchi wakaweza kuhimili kulima kutumia mabonde hayo?

Tukielewa nchi yetu ni kisiwa, ardhi yetu ni ndogo, na hivyo ilivyo sasa inavamiwa na maji. Sasa kama hali hiyo fedha hizo hazikupatikana kwa utaratibu huwo, maana yake tunaendelea kuzalisha wananchi wetu wanaoishi katika mazingira magumu, hiyo miradi iandaliwe iwe mingi zaidi, ndiyo maana yake. Si tuna miradi ya kuhami hizo Kaya masikini, basi nasema kwamba itakuwa hivyo. Wanaoathirika na haya ni wakulima zaidi ni wanawake, ndio wakulima na ndio wazalishaji wakubwa wa Taifa hili katika kilimo ni wanawake. Mheshimiwa, naomba nipate hilo jibu nilidhani Waziri wa Fedha atakuwepo niweze kupata kidogo lakini bahati imekuwa mbaya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nije kwenye ukurasa wa 9 katika kifungu hichi cha 30 kwenye madawa ya kulevya. Niseme kwamba Taifa kwa wakati huu lina asilimia kubwa sana ya vijana ambao ndio nguvu kazi ya Taifa letu. Madawa ya kulevya yameathiri mno hali ya uzalishaji wa Taifa, kwa sababu vijana wetu wengi wamejitumbukiza huko, hali haipo shuwari. Wakijitumbukiza huko mbali na matatizo mengine ya kwamba wao sasa wawe ndio wenye kuhudumiwa badala ya

kwamba tutumie nguvu zao kwa ajili ya kuzalisha zaidi. Lakini pia kuna mambo mengine yanapatikana, kuna mambo ya Ukimwi.

Nalo nilisema kwamba taasisi hii ni mtambuka, mambo yake yote yanagusa jamii kwa pamoja. Kwa hivyo, tunaona kwamba tumeanzisha ujenzi wa kituo cha tiba cha marekebisha ya tabia, lakini nayo pia kipindi kilichopita bajeti yenu haikuingizwa na sasa hivi tuko kwenye *PBB*, nikasema kwamba Mhe. Waziri wa Fedha alikuwa awepo naye atupatie kidogo kwamba kwa sababu makusanyo tunaambiwa kwamba yaliongezeka na mambo mengine yamekwenda hivyo.

Je, tutatumia miaka mingapi kujenga kwa sababu kutafuta kiwanja tumetumia miaka kadhaa, tumepata kiwanja tumeanza lakini fedha kulingana na uhisani tunaoupata pamoja na misaada ya kibajeti ambayo kwa awamu iliyopita mwaka huu wa fedha huu unaomalizika hazikupatikana fedha hizi. Sasa tuna mashaka inawezekana ikawa ndio yale ya kuuziwa ng'ombe kwa mlio jamani, ikawa tunaambiwa na matokeo yake yakifika mwaka huo ukiingia wa bajeti tunakaambiwa fedha hazikuingizwa, kwa hivyo, hayandio mashaka yangu makubwa ambayo mimi ninayo.

Jengine ni kwamba haya tunayoyafanya tuliwahi kujifanyia tathmini sisi, vijana ambao wameweza kuathirika na madawa ya kulevya tangu mwanzo ambapo tumegundua madawa haya na wakati huu tuko wapi na ni vijana wangapi wanaambukizika katika kipindi hiki, yaani wanaunga mkono hii kuingia katika haya madawa ya kulevya na kwa sababu tunafanya juhudi kwa wakati huu tupo wapi ili tuweze kujua tunafanya haya tunaelekea wapi na tunapambana na watu wa kiasi gani. Mimi sidhani kwamba mmewahi kufanya *research* hiyo, hebu fanyeni mtupe hiyo tathmini mliyonayo tuone tunaelekea wapi. Tunaona kwamba zinatolewa fedha, maelekezo na mambo mbali mbali, lakini tukijitathmini tulivyoanza, tulipo na huko tunakoelekea tukoje, jamani lazima tuende hivyo tusije tukaletewa haya manamba tu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika huu uharibufu wa mazingira. Wenzangu walizungumza katika utaratibu tofauti tofauti, nami nasema kwamba uharibifu huu wa mazingira lazima tujielewe kwamba sisi chetu ni kisiwa na nilisema hapa katika kipindi cha nyuma kilichopita kwamba ardhi yetu pia nayo inahitaji kugaiwa tukajua ardhi ya kilimo, ardhi ya uwekezaji, ardhi ya majenzi, lakini bado kumekuwa na vurugu mechi, kibali anatoa mtu wa misitu lakini mtu wa mazingira anaambiwa wewe ulinde, akilinda mambo hayawi. Kuna sheria imetengenezwa na tumeipitisha sisi hapa, lakini mwanzo nilipokuwa naanza kuchangia nilisema kwamba tuna matatizo ya usimamizi wa sheria. Inaweza ikaja hiyo sheria lakini isiweze ku-*function*, yaani isifanye kazi yoyote kwa sababu tuna mazoea mabaya.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo ninaiacha hapo kidogo ili nije kwamba hata na uchimbaji wa mchanga na mawe tuwe utaratibu basi maalum wa kuona hayo maeneo tunayoyatumia yanakubalika, yako sawa na athari zake ni nini hawa watu wafanye hiyo shughuli yao watu wa mazingira lakini hakuna hilo. Pakiamuliwa basi mambo yanakuwa hivyo.

Jengine ni hizi mali chakavu ambazo zinaletwa, yaani makarakacha, Zanzibar sasa imekuwa ni jaa la kutupia mataka taka, mali kachara zimekuwa nyingi ambazo wakati mwengine hazina haja imekuwa madubwana ambayo yanaleta uchafuzi wa mazingira katika nchi yetu na kisiwa chetu ni kidogo, hebu tuangalieni na hilo nalo jamani huko bandarini yanapopitishwa tukayatizama haya madubwana, Mhe. Omar Yussuf ambaye nilikuwa nataka ajuwe yeye anakusanya kodi tu haoni kuna athari nyengine hizi ambazo kwamba vinaletwa hivyo vitu vina athari, haoni hili, isiwe kodi ambayo tunatoa lakini ikawa ina athari kubwa kwetu kwa Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, narudi tena hapo hapo nikirudi kwenye uwekezaji, wawekezaji wetu tunasema kwamba tunahitaji uwekezaji kweli na lazima tufanye hilo ili tuweze kuinua kipato kwa ajili ya kufanya shughuli zetu za maendeleo katika Taifa. Lakini sasa umefika wakati wa kuona basi hao wawekezaji wetu wanafuata taratibu tulizoziweka sisi wenyewe nchini, tunashindwa kufuata sheria tatizo. Nimeshuhudia mimi na kamati yangu katika ujenzi wa hoteli moja kule Makangale, Mhe. Mwenyekiti wa Kamati yangu alikataa katakata akasema jamani hali hii si nzuri ibadilisheni msifanye hili, wakasita kidogo hatimaye vigogo wamekwenda wanasema iendelee tumekuta imejengwa ufukweni ndio vigogo.

Nauliza sheria ya nchi hii ni kwa wanyonge tu, ni watu waliokuwa hawamudu tu, vigogo waendelee kufanya shughuli zao. Nasema tena tumetengeneza sheria na sheria ni msumeno sheria inawagusa watu wote wa Taifa hili na kama hatukufanya hili kwa kuzingatia tukisema tunafanya kwamba aliyekamatwa ni mwenye gari moja la mchanga lakini wale wanaofanya uharibifu mkubwa wa mazingira kwa sababu ya ukubwa wao wakiwa wanaachiliwa, nasema kwamba hatutendi haki na sheria haitakuwepo na wao hatimaye watagoma hili.

Nasema kwamba sheria ifate mkondo vigogo hawa ambao wameruhusu hoteli hiyo kujengwa huko ndani ya ufukwe kabisa, jamani si utaratibu mzuri. Mimi binafsi nilikuja na hoja humu ikatolewa na Mhe. Hija Hassan Hija ya ukataji wa miti kiholela wakati wa ujenzi wa Kiwanja cha Gofu hapo Nyanjale; ilikatwa mifenesi, midoriani, mishoki shoki, kila kitu mpaka mikoko imekatwa na imejengwa barabara ya kifusi badala ya kwamba watu wa mazingira walikwenda wakagundua, Mhe. Spika, aliunda Kamati na fedha za walipa kodi tulizitumia, ripoti hiyo haikusomwa humu maana vigogo hawakutaka, haikujulikana mbichi wala mbivu tumetulia tu kimya hakuna kilichoendelea, maana yake kwa nini kuna vigogo.

Nasema hivi kwamba sheria zifuate mkono hayakusemwa. Maji yamefukiwa na mikoko imekatwa kimya kabisa hali imeendelea, kama tutaendelea hivi hatutofika.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja tena hata tathmini ya kimazingira miradi kadhaa haijafanyiwa tathmini hiyo ila iliyofanyiwa ni miradi michache. Hebu jamani tuangalieni hizi athari za kimazingira ambazo sisi zinatuathiri, tusipoziba ufa nasema tena tutajenga ukuta.

Jengine ninakuja kwenye ukimwi, nasema kwamba nimesikitishwa na kitabu hiki Mhe. Waziri, ulipoandika kwamba umewafikia madada poa na makaka poa, nauliza mila na tamaduni za Wazanzibari ni kuhalalisha dada poa na kaka poa. Hili ni jambo ambalo ninasikitishwa kwamba kuna fedha zinatumika eti kuna dada poa na kaka poa, mila na tamaduni za Wazanzibari haziruhusu haya, ikiwa mnayaandika katika vitabu vya Serikali mnakusudia kusema nini?

Utamaduni wa Taifa ni raslimali, tamaduni zetu haziruhusu haya kama mnatumia kwa madada poa na makaka poa raslimali zetu nasema mnakwenda kinyume mila na tamaduni zetu au hamthamini tena udamaduni wetu, kwamba wageni wanaokuja hapa wanatamani waige mila na tamaduni zetu, sisi haziruhusu. Leo sisi tunaandika kwenye vitabu hivi tumewafikia dada poa 150 na kaka poa 150 tamaduni ya Zanzibari hairuhusu hili jamani, ndio ukweli na lazima tuseme hili. Jamani tulitarajia vitu vyengine, hao dada poa, kaka poa na ukimwi maana yake umeruhusika na miziki inapigwa halafu tunatumia *lot of money* kwa mambo ambayo tungeweza kutumia tamaduni zetu, tungeweza kuokoa fedha za Serikali tukafanya shughuli nyengine za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maneno yangu hayo kwa kuwa nami ni mjumbe wa kamati hii, ni mdau humu nasema naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante ninakushukuru.

**Mhe. Amina Idd Mabrouk:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia asubuhi hii ya leo tukiwa wazima na afya njema. Lakini pia nichukuwe nafasi hii kukushukuru wewe Mwenyekiti kwa kunipatia fursa hii adhimu ili na mimi niwe mchangiaji wa bajeti hii muhimu kwa Taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nichukuwe nafasi hii ya pekee kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa namna wanavojitahidi katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inapiga hatua. Lakini zaidi nichukuwe nafasi hii adhimu na ya pekee kumpongeza Mhe. Waziri wa kuwa mwanamama na kazi zake anazifanya vizuri basi nichukuwe nafasi hii nimpongeze sana na ninaamini kwamba kinamama tunaweza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu hautokuwa mkubwa kama ulivyosema na nitaheshimu maamuzi yako kwamba muda tusitumie mrefu ili na wengine waweze kupata nafasi ya kuchangia.

Nianze katika ukurasa wa 13 wa kitabu hiki, ujenzi wa mradi wa kituo cha marekebisho na tabia kwa watumiajiwa madawa ya kulevya. Mimi Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri na Serikali kwa ujumla kwa kuona kwamba upo umuhimu mkubwa wa ujenzi wa kituo hiki cha vijana wetu. Lakini pia nichukuwe nafasi hii adhimu kabisa kuwapongeza wale watu binafsi ambao walianzisha vituo hivi vya *Sober House.*

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, wale watu ambao walianzisha vituo hivi waliifanya kazi hii ya kujitolea, lakini pia waliifanya kazi hii kwa imani kubwa walikuwa nayo na sio kwa ajili ya biashara. Hii inaonekana kwamba Mhe. Mwenyekiti, wale watu ambao walianzisha vituo hivi waliona kwamba sasa hivi Taifa letu linateketea kwa vijana wetu kwa utumiaji wa madawa ya kulevya. Na walifanya kazi hii katika mazingira magumu sana Mhe. Mwenyekiti, lakini hawakurudi nyuma na waliendelea kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata hifadhi ile.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Serikali ndio ilikuwa ina wajibu mkubwa wa kuona kwamba vijana wetu hawa walioathirika na madawa ya kulevya wao ndio wanawapatia hifadhi na kuona kwamba zile tabia wanazirekebisha za vijana wetu. Lakini mimi nishukuru sana kuona kwamba ndani ya kitabu chake hiki Mhe. Waziri, ametwambia kwamba ujenzi wa kituo hiki kinaendelea kule Kidimni. Kwa kweli wananchi wakisikia hivi sasa sisi wazazi tunafarijika sana na tunaona kwamba Serikali yetu inawajali vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi basi mimi nitoe masikitiko yangu makubwa kuona kwamba ujenzi huu umetengewa asilimia 18 tu ya pesa. Kwa kweli huko nje vijana wetu wanateketea kwa hali kubwa sana. Sasa mimi nilitegemea kwamba kitabu hiki tuone kwamba asilimia ya pesa itakayotumika angalau inaridhisha. Mhe. Mwenyekiti, na hali hii inavyoonesha kwamba hata miaka 5 hii ikipita basi ujenzi huu inawezekana ukawa haujamaliza kujengwa.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, nisema kwamba Serikali itilie mkazo mkubwa kuona kwamba kituo hiki kinapiga hatua na vijana wetu wale wanapata hifadhi. Lakini pia niiombe Serikali kwa ujumla Mhe. Mwenyekiti, ione kwamba hapo baadae ujenzi wa vituo vyengine kama hivi ili kuona vijana wetu wanapata hifadhi. Ninasema hivi Mhe. Mwenyekiti, kwa kuona kwamba sasa hivi hakuna kijiji hata kimoja ambacho hakina waathirika wa madawa ya kulevya. Kwa hivyo, mimi niseme kwamba tuwapunguzie mzigo wa kuongeza vituo hivi vya madawa ya

kulevya vya kuwabadilisha vijana wetu tabia ili tuwarahisishie vijana wetu kutokwenda mbali.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, niendelee katika ukurasa wa 19 *operation* wa mifuko ya plastik. Mimi Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii kuipongeza Idara hii ya Mazingira kwa kazi nzuri inayofanya ya kupambana na uingizajiwa mifuko ya plastik hapa Zanzibar. Lakini Mhe. Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi nimeshtushwa sana kuona kwamba bado uingizaji wa mifuko hiyo ni tishio kubwa na matukio 33 mwaka hii Mhe. Mwenyekiti, inatisha hasa tukizingatia kwamba kisiwa chetu hiki cha Zanzibar kina watu kidogo mno.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilijiuliza hivi inakuwaje kwamba kwa mwaka matukio 33 wamekamatwa watu wamepitia wapi? Mhe. Waziri, aje kutwambia. Kwa sababu mimi ninaamini kwamba sehemu ambazo za usafiri ni bandarini na *airport.* Sasa hivi vyombo vya usalama vipo wapi hata kuona kwamba matukio kama haya yanakuwa makubwa, kwa kweli hili ni tatizo kubwa. Kwa sababu asilimia hii 33 inaonesha kwamba kwa mwezi matukio kwa kweli yapo mengi.

Lakini mimi niseme kwamba Mhe. Mwenyekiti, tulipitisha hapa sheria ambayo ya kudhibiti uingizaji wa mifuko hii ya plastik. Sasa Mhe. Mwenyekiti, unapoona tatizo hili limekuwa kubwa na imani yangu kwamba inawezekana kwamba haya matukio ndio ambayo nimeripotiwa, lakini inawezekana kwamba kuna mifuko mengine imo ndani ya nchi yetu lakini Serikali haina taarifa nayo. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kwamba hili tatizo linahatarisha amani ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea niseme kwamba watu hawaogopi sheria iliyopo ya kudhibiti uingizaji wa mifuko ya plastik na sababu ya kutoogopa mimi niseme kwamba labda pengine sheria iliyokuwepo haina adhabu kali. Ndio maana mtu anajua atafanya, atakamatwa na hatimaye atapewa hiyo adhabu ambayo sio kubwa, kwa maana hiyo haogopi kuingiza mifuko hii ya plastik.

Pia, Mhe. Mwenyekiti, inaonekana pia hii sheria iliyokuwepo au hili zoezi zima la kuhakikisha kwamba tunaitekeleza hii sheria kwa vitendo inawezekana ni dhaifu. Kwa hivyo, mimi niiombe Idara ya Mazingira kujidhatiti kuona kwamba wanasimamia sheria ambayo tumeitunga wenyewe pamoja na sera zake.

Mhe. Mwenyekiti, waliotangulia hapa walisema kwamba tatizo tulilokuwa nalo kwa kwetu hapa Zanzibar sheria hazifatwi, sheria hazitekelezwa, kwa hivyo, watu hawaogopi kuvunja sheria. Niiombe Serikali kwa ujumla tuhakikishe kwamba tunazisimamia sheria tulizozitunga wenyewe na kuzipitisha katika Baraza letu hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nije katika ukurasa 26 kuratibu na kudhibiti madawa ya kulevya. Mhe. Mwenyekiti, hili tatizo wenzangu wengi hapa wamelizungumza kuwa tatizo la madawa ya kulevya ni tatizo kubwa na vijana wetu siku hadi siku wanateketea kwa tatizo hili la madawa ya kulevya. Na mimi niseme kwamba Serikali haijawa *serious*, lazima serikali iwe *serious* katika kuhakikisha kwamba tunazuia uingizaji wa madawa ya kulevya nchini kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, hiki kisiwa ni kidogo sana, kwa maana hiyo basi tunao uwezo mkubwa, serikali ina mikono mingi, kwa hiyo, nina hakika tukipania kuhakikisha kwamba tunazuia uingizwaji wa madawa ya kulevya, ninaamini kwamba hatutofikia hii hatua tuliyofikia. Lakini kila tukija hapa tunaambiwa kwamba madawa ya kulevya yanaongezeka na vijana wetu wanateketea kwa madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuombe Mhe. Waziri, tufanye kazi ya ziada kuona kwamba tunatoa elimu maskulini juu ya suala zima la madawa ya kulevya. Na ninasema hivi Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hali halisi inaonekana kuwa vijana wetu ndio wanaojingiza katika madawa ya kulevya, lakini zaidi ni watoto, kwa sababu wale watoto ambao wanatoroka maskulini wanaranda mitaani, ndio wale wale inawapelekea kuingia katika suala zima la madawa ya kulevya.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa, umebakiza dakika tano, malizia.

**Mhe. Amina Iddi Mabrouk:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Kwa hiyo, mimi nimuombe Mhe. Waziri, tufanye juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba tunatoa elimu maskulini kwa vijana wetu katika suala zima la athari za madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala la ukimwi. Mhe. Mwenyekiti, ukimwi unaua na ukimwi hasa ni vijana wetu ndio wanaathirika katika suala zima hili la ukimwi, hasa hasa ni vijana wetu ambao wanatumia madawa ya kulevya kutokana na utumiaji wa madawa hayo katika njia za kujidunga kwa njia ya sindano. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, wenzangu walitangulia kusema hapa; "usipoziba ufa utajenga ukuta".

Kwa hiyo, mimi niseme Mhe. Mwenyekiti, tusipoliangalia suala hili la uingizaji wa madawa ya kulevya, mimi ninaamini kwamba na suala la ukimwi litatushinda kulizuia, kwa sababu sasa hivi mimi ninamuomba Mhe. Waziri, atapokuja kutoa majumuisho atwambie vijana wangapi ambao walioathirika na madawa ya kulevya waliokuwa na tatizo la ukimwi, ni asilimia ngapi? Naamini kwamba sasa hivi huko

nje hali sio shuwari, vijana wetu wengi wanaingia katika suala zima la madawa ya kulevya, lakini vijana wengi wanaathirika na madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nichukue nafasi hii pia kuipongeza serikali kwa namna ilivyojitahidi katika kuhamasisha namna ya kuwanyanyapaa wagonjwa wa ukimwi. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana na imepungua ya unyanyapaa wa wagonjwa wa ukimwi. Sasa hivi mgonjwa wa ukimwi anaishi kwa raha tofauti na kipindi cha nyuma, kwa hiyo, mimi naamini kwamba serikali ikijidhatiti katika suala hili pia la madawa ya kulevya inaweza, "tutimize wajibu wetu".

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa kumalizia kusema nichukue nafasi hii kuipongeza serikali, kumpongeza Mhe. Waziri, kwa kazi nzuri anayoifanya na nimalizie kwamba naiunga mkono hotuba hii asilimia 99. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kukushuru kwa kunipa nafasi hii ili angalau na mimi nikachangia kwenye hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Nitangulie kwa kumpongeza kwa dhati Mhe. Waziri, kwa mawasilisho yake ya hotuba hii, na kwa namna kwa kweli anavyoisimamia wizara katika suala zima la kutekeleza majukumu yake siku hadi siku. Pia, nielekeze pongezi zangu kwa Katibu Mkuu pamoja na kikosi kazi chake cha watendaji katika ofisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, tunayoijadili leo ni Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, ni moja kati ya ofisi tatu kubwa katika nchi yetu. Ni Ofisi ya Makamu ya Kwanza wa Rais ambayo inaongozwa na yeye mwenyewe Makamu wa Kwanza wa Rais, ni ofisi muhimu sana kwamba yeye mwenyewe ni Mshauri Mkuu wa Rais. Lakini pili, ofisi hii imeundwa na idara muhimu sana, ni idara muhimu lakini bahati mbaya sana ni idara ambazo hazionekani, umuhimu wake hasa hauonekani. Na hauonekani kwa sababu yawezekana kwamba hazigusu yale maisha tunayoyahisi sisi kwamba ni maisha ya siku hadi siku tofauti na wizara nyengine, ama tofauti na idara nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze na Idara ya Mazingira. Idara ya Mazingira ni idara muhimu sana kwamba katika Idara hii ya Mazingira tunataraji kuwa kule kunaratibiwa kwanza suala zima la utunzaji wa mazingira na suala la uhifadhi wa mazingira. Tumefahamu athari ya uharibifu ama uchafuzi wa mazingira katika maisha ya siku hadi siku. Katika nchi zilizoendelea suala hili la uchafuzi wa mazingira kutokana na maendeleo, maendeleo ndio yanayopelekea uchafuzi wa mazingira. Lakini bahati mbaya nchi za dunia ya tatu, ama nchi hizi za Kiafrika na nchi nzima za dunia ya tatu kwa kweli suala la uharibifu wa mazingira Mhe. Mwenyekiti, linasababishwa na suala la maisha tu ya kila siku. Suala la maisha ya kila siku ndio yanayopelekea uharibifu na uchafuzi wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, uchafuzi wa mazingira mara nyingi husababisha maradhi, sasa hivi wale wakaguzi wakuu wa serikali zote za dunia zimetakiwa zifanye ukaguzi maalum unaohusiana na suala zima la uchafuzi wa mazingira. Kwetu sisi hatulipi umuhimu, hatulipi umuhimu kwa sababu hatuangalii ama hatuzingatii zile athari hasa zinazopelekea yatokanayo na uharibifu wa mazingira.

Ndio maana siku hizi kuna kitu kinachoitwa *environmental auditing*, ni kutokana na athari zake katika suala zima la uchumi wa nchi, ndio kukatolewa umuhimu huo na kipaumbele hicho kwamba wakaguzi na wadhibiti wakuu wa mahesabu wafanye ukaguzi huo. Kwa hivyo, suala zima linalohusiana na uchafuzi Mhe. Mwenyekiti, hupelekea kuwepo kwa maradhi ya mripuko na hili tunafahamu kwamba athari yake ni kuwa serikali hutumia fedha nyingi sana katika kukabiliana na suala hili, suala la maradhi ya miripuko na maradhi mengine.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile suala la uharibifu wa mazingira hupelekea suala la ukame, suala la ubadilikaji wa miongo ambayo tunafahamu kwa kila mmoja athari zitokanazo na matatizo hayo kwamba kilimo huathirika na tukisema kilimo huathirika, uzalishaji katika kilimo lakini vile vile suala zima la upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya viumbe. Kwa hivyo, kwa vyovyote vile suala la uchafuzi na suala la uharibifu wa mazingira linaathari kubwa sana, sana katika suala zima la uchumi wa nchi. Inapaswa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itanabahi na ilitilie umuhimu sana suala zima linalohusiana na utunzaji, suala zima linalohusiana na uchafuzi pamoja na uharibifu wa mazingira kwa sababu linaathari mbaya sana katika masuala ya maendeleo pamoja na suala zima la uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, sisi wananchi ama sisi wawakilishi wa wananchi tulikuwa ama tuna matazamio katika bajeti hii. Mhe. Mwenyekiti, mimi leo sitojikita sana katika suala zima linalohusiana na utolewaji wa fedha katika idara hizi. Leo nitachangia katika suala zima linalohusiana na mfumo wa hii bajeti mpya pamoja na vipaumbele tunavyoviweka kama serikali, kwa sababu sisi matazamio yetu ni yepi? Matazamio yetu ni kuwa na *programme* hii kama ilivyoelezwa kwamba tuna *programme* inahusiana na suala zima la uhifadhi wa mazingira. Ikiwa hiyo ni *programme* ndani yake tunataraji kutakuwa na yale mambo ambayo yanayopelekea kuharibika kwa mazingira, ili serikali ipambane na iweke kipaumbele katika sekta zile. Kwa mfano, tumeona kwamba moja ya kitu kinachosababisha uharibifu wa mazingira Mhe. Mwenyekiti, ni suala la kutokuwa na ajira vijana.

Suala la kutokuwa na ajira sasa hivi limepelekea watu kuchimba michanga, limepelekea watu kukata miamba kwa ajili ya matufali, limepelekea watu kukata miti ovyo, limepelekea watu kufanya *destruction* tofauti, tofauti, tofauti. Leo ajabu watu wa Giningi, Giningi nafikiria Mhe. Mwenyekiti, unakufahamu, leo Giningi takriban mchanga wote ule ushachukuliwa, watu wanafukuwa sijui hata wenyewe

wako akina Mhe. Mohammed Mbwana, hapa, maana yake ni ajabu watu waende Giningi tu wakachafue ardhi za watu na nini na nini na watu wanaangaliwa tu.

Lakini yote ni kwa sababu wananchi pamoja na Kaskazini kule Bumbwini na sehemu nyengine Donge yote hiyo ni kwa sababu watu hawana ajira. Kwa hivyo, tulitaraji serikali iwe na *programme* ingawa hapa hatuitazamii Ofisi ya Makamu wa Kwanza kwa sababu sio inayozalisha ajira, kwa sababu suala la ajira ni suala mtambuka. Tulitaraji katika wizara zinazohusika kama uwezeshaji na wizara nyengine ziwe na *programmes* maalum zinazohusiana na suala la ajira, kwa sababu vijana wakipatiwa ajira za uhakika haya mambo ya uharibifu wa mazingira yakukata miamba pamoja na uchafuzi wa kuchimba michanga kwa kiasi kikubwa Mhe. Mwenyekiti, itapungua. Kwa hivyo, moja kati ya jambo linalosababisha uchafuzi wa mazingira ama uharibifu wa mazingira ni suala la ajira. Kwa hiyo, tulipaswa tuwe na *sub-programme* inayohusiana na suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili au hili hili la ajira ilikuwa wizara inayohusika hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais iwe na *sub-programme* ya kuratibu ajira katika wizara zinazohusika kwa sababu hili ni jambo mtambuka katika wizara nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jambo hili la pili katika bajeti hii tulitaraji kuwe na *sub-programme* inayohusiana na uhifadhi wa mazingira, uhifadhi wa vyanzo vya maji, humu jambo hilo sijaliona kama wizara inayohusika ama inayosimamia suala hilo hili sijaliona katika bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine nilitaraji kuwe na *sub-programme* inayohusiana na *programme* ya uvuvi endelevu. Kwa sababu katika suala linalohusiana na uharibifu wa mazingira baharini na sehemu nyengine ni suala la kutokuwa na uvuvi endelevu. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile wizara hii kwa sababu ndio inayosimamia hilo kulikuwa kuwe na *sub-programme* kinachofuatilia utekelezaji wa jambo hili katika wizara inayohusika, kwa sababu nasema kwamba hii ni wizara inayosimamia lakini mtekelezaji wa athari hiyo haitokani na wizara hii, ni wizara inayohusika na mambo ya kilimo, wizara inayohusika na mambo ya uvuvi, wizara inayohusika na mambo ya maji, wizara inayohusika.

Kwa hiyo, hili ni jambo mtambuka lakini kama ni wizara inayosimamia kulikuwa kuna *programmes* ambazo zinahusiana na suala hilo. Lakini sikupata jibu katika bajeti hii, na nikisema katika bajeti hii nilitaraji katika hizi *activities* ambazo nimepewa hamna kitu kinachohusiana moja kwa moja kwenye eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la pili, madawa ya kulevya. Mhe. Mwenyekiti, hakuna leo aliyekuwa hajui athari zinazotokana na madawa ya kulevya, kwa sababu tulisema siku nyingi na kila mmoja anajua kwamba madawa

ya kulevya yanaathari kubwa ya kuua nguvu kazi ya Taifa letu, hasa vijana takriban wengi sana sasa hivi hasa katika maeneo ya Mijini na bahati mbaya sana hata maeneo ya vijijini siku hizi kuna masuala yanayohusiana na madawa ya kulevya. Yana athari sana sana kama nguvu kazi ya vijana ambao ndio wazalishaji wakubwa sana katika Taifa letu.

Matarajio yetu nini katika bajeti hii? Katika bajeti hii Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nikitegemea kwamba kutakuwa na *sub-programme* mbili kubwa, maana yake tusiongee mambo tu kijumla jumla, bajeti zetu hizi zinaongea mambo kijumla jumla. Mimi nilikuwa nategemea kwamba bajeti hii ilikuwa iwe na *sub-programmes* mbili ukiachia mbali hii *programme* kubwa; Kuwe na *sub-programme* yakupambana na uingizaji wa madawa ya kulevya, ingawa narudia tena kwamba Wizara ya Makamu wa Kwanza haiwezi kulitekeleza jukumu hili. Lakini hii Ofisi ya Makamu wa Kwanza ilikuwa ndio msimamizi na mratibu wa suala hili hasa katika vyombo vya ulinzi na usalama.

Mhe. Mwenyekiti, hili sikuliona na hata nikaliona kama limo lakini ni bahati mbaya sana serikali bado haijawa na majibu juu ya uingizwaji wa madawa ya kulevya. Basi kama ni vita niseme kwamba serikali imeshindwa na vita hii. Serikali imeshindwa na vita hii na mimi siamini pahala penye serikali makini yenye vikosi vingi ikashindwa na suala zima la uingizaji wa madawa ya kulevya, haiyumkiniki na wala haiwezekani.

Mimi niamini tu kwamba ni kutokana na serikali wenyewe kwamba haiko makini katika suala hili, na hapa ndipo zinapokuja shutuma nyingi kwamba na vigogo nao watakuwa nao wana mikono yao katika hili. Kwa sababu hadi leo madawa ya kulevya yanaingia na hii inawezekana, ikiwa tumepambana na ofisi imepambana kwa kiasi kikubwa na kuingiza mifuko ya plastiki kwa kiasi kikubwa imepungua, ilikuwa ikiingizwa kwa magendo hii, itakuwaje leo serikali ishindwe kukabiliana na uingizaji wa madawa ya kulevya?

Kwa hiyo, sisi wananchi hatuwezi tukaelewa lolote kama serikali haikutupa jibu namna gani inavyopambana kivitendo na suala la uingizaji wa madawa ya kulevya katika nchi yetu. Hakuna lugha ambayo tunaweza tukaifahamu katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ukiachia mbali *programme* inayohusiana na uingizaji wa madawa ya kulevya chengine ambacho tulikuwa tunategemea kiwemo katika bajeti hii kama *sub-programme* ni suala la kuwasaidia wale walioathirika na madawa ya kulevya ili kama ni tiba ama vyovyote vile ilikuwa kuwe na *programme* tuione hapa, *sub-programme* tuione. Kwa sababu tayari wapo watu sasa hivi wameathirika na madawa ya kulevya, je, serikali inawasaidia nini?

Na serikali kuwasaidia hiyo tumeona kama kuna *Sobha House*, *Sobha House* kipindi cha nyuma hiki takriban watu binafsi tuna mashirika ya kijamii ndio yaliyokuwa yakijitokeza. Je, serikali inaweka mkono gani, maana yake hili suala haliwezekani tu lichukuliwe na watu binafsi wakati serikali ipo. Leo serikali kwenda kuchangia milioni moja ama milioni mbili katika jambo hili zito hatuoni kama linafanya jambo la maana sana. Hili jambo kwa asilimia mia moja tulitarajia kwamba serikali tayari ilichukue kama ni janga la kitaifa. Lakini leo katika *programme* hii hakuna kitu kilichokuwa kinakwenda moja kwa moja.

Kwa hivyo, tulitaraji kuwe na *sub-programmes* mbili, moja ni kupambana na uingizaji wa madawa ya kulevya, lakini la pili ni kuwasaidia wale ambao tayari wameathirika ili kuachana na sikuachana tu Mhe. Mwenyekiti, karibuni mimi tulikuwa tunae kijana mmoja aliacha kwa muda, kuna vijana tu walimshawishi mwenzao akaacha kwa muda. Lakini baada ya miezi miwili Mhe. Mwenyekiti, alikuwa mtu mzuri kwa kweli mswalihina sana, alikuwa ni mswalihina sana, lakini alivyoachiliwa kidogo leo amerudia kule ukimkuta ni nyang'anyang'a. Maana kumbe vile suala hili linahitaji liwe ni endelevu kwamba mtu umtoe lakini ukishamtoa umuweke *busy,* ama umfanye umjengee mazingira yakumfanya yeye asirudie tena kule.

Hiki ni kitu muhimu sana Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, hizi *programmes* nilikusudia kuziona, nilitaraji kuziona katika bajeti hii ili tuone kwa sababu ikiwa madawa hayatoingizwa na ikiwa wale walioathirika watafanywa *treatment* ama watapatiwa ajira tunaweza tukafikia madawa ya kulevya ikawa ni *zero* katika nchi yetu, upo uwezekano mkubwa kabisa madawa ya kulevya ikawa ni *zero* iwapo mambo hayo mawili yatachukuliwa. Kwa hivyo, bajeti hii mimi binafsi ilikuwa nataraji mambo hayo mawili.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la tatu ni suala zima linalohusiana na maradhi ya ukimwi, vile vile, hakuna mtu ambaye hajui athari zitokanazo na ukimwi, kwa sababu ukimwi unaua nguvu kazi ya Taifa ambayo ndio wazalishaji na wachangiaji wakubwa wa maendeleo. Iwapo ukimwi kwa kweli hatutouchukulia hatua Mhe. Mwenyekiti, Taifa letu litakuwa ni Taifa la wagonjwa, wote watakuwa wagonjwa; viongozi, wanachama na nani hawa wote watakuwa ni wagonjwa tu. Kwa hivyo, ni jukumu la serikali kuwa makini mno katika suala la kupambana na ukimwi. Na katika hilo basi, nilikuwa nataraji katika bajeti hii pia kwamba kuwe na *sub-programme* yakupambana na maambukizi mapya. Hii ni *sub-programme* ambayo nilikuwa nataraji kuiona.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili nilikuwa nataraji kuona *sub-programme* inayowasaidia wale ambao wameathirika, kuwasaidia moja kwa moja. Humu imeandikwa kwamba kuwasaidia wanawake wenye Virusi vya UKIMWI,

walioathirika sio wanawake tu na wanaume wamo, lakini hicho walichokijali ni kitu gani. Katika bajeti hii fungu hili ambalo lilikuwa linakwenda kwenye shilingi bilioni moja mia saba na tatu, eti fedha iliyotengwa ni shilingi milioni mbili, *just imagine*, maana yake wale walioathirika ambao ndio tulikuwa tunafikiria sisi mtakwenda kuwasaidia angalau wapate lishe, angalau waweze kujiajiri waendeshe familia zao, leo humu kilichoandikwa ni shilingi milioni mbili ambacho ndio kilichopangwa tena wanawake peke yao, shilingi milioni mbili kwenye bajeti hii. Lakini sasa tuone hii bajeti nyengine yote inakwenda wapi.

Mhe. Mwenyekiti, nilichojifunza katika serikali ni hiki, kwamba Mwenyezi Mungu huleta haya mambo lakini ikawa ndio sababu ya kuwatafutia watu chejio, humu ni chejio tu fedha zote hizi zimekwenda kwenye warsha, kwenye makongamano kwenda kuchapisha, hilo sio lengo letu, lengo letu kama ni waathirika wa UKIMWI wasaidiwe waathirika wa UKIMWI wenyewe.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa, umebakisha dakika tano kumalizia.

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Bado tano, ee sawa, basi naomba niseme la mwisho. Mhe. Mwenyekiti, la mwisho, ni suala zima la wenzetu wenye ulemavu. Walemavu hawa Mwenyezi Mungu kawajaalia na sisi kila mmoja hatujui tutamalizia vipi, kwa sababu watu wanasema ile kumalizia ndio muhimu, sisi hatujui kesho na keshokutwa tutakuwaje. Kwa hivyo, kwa sababu hiyo ilikuwa tunataraji kwa vyovyote serikali iweke umuhimu kwa suala zima la watu wenye ulemavu ili tuone kwamba nao wanakuwa na mchango mkubwa katika suala zima la ujenzi wa Taifa letu.

Sasa katika hili tulikuwa tunataraji kuwe na *sub-programme* vile vile ya kuwasaidia na kuwawezesha watu wenye ulemavu. Kwa sababu mtu akishalemaa lazima Mwenyekiti ni muhimu sasa kwa serikali kumsaidia katika nyanja mbali mbali, vile vile ni suala mtambuka apate elimu. Lakini watu wenye ulemavu wasaidiwe katika ajira kwa sababu na wao ni watu ambao wanahitaji mapato, vile vile, watu wenye ulemavu wasaidiwe fursa nyengine pamoja na suala zima la kujiwezesha.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile serikali ilikuwa iwe na *sub-programme* ya kuwasaidia watu wenye ulemavu kwa sababu ulemavu mwengine ni ulemavu unaopatikana na uzembe wetu wanadamu. Kwa hivyo, hili leo tulizungumziwa kwamba kila sekunde 20 duniani mguu wa mtu mmoja hukatwa kutokana na maradhi ya kisukari, ndio takwimu za dunia hizo, kila sekunde 20 dunia hukata mguu wa mtu mmoja,  sasa angalia vilema wa miguu hao, pengine atakatwa mguu huu na mwengine huu. Sasa kupambana na maradhi kama ya kisukari mtu mwenye

maradhi ya kisukari hupata ulemavu wa macho huwa haoni, mtu mwenye kisukari hupata ulemavu mwengine akawa hazai vizuri. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kwa vyovyote vile serikali ilikuwa iwe na *sub-programme* ambayo ni mtambuka katika wizara zinazohusika hasa Wizara ya Afya, wizara inayohusiana na mambo ya usalama barabarani na vitu vyengine. Tukifanya hivyo tunaweza tukafika pahala tukapunguza kwa asilimia kubwa walemavu katika nchi yetu, lakini vile vile wale waliokuwa washakuwa walemavu serikali ikawa na mpango wa kuwasaidia katika maisha yao na hivyo nao wakajiona ni sawa na wenzao ambao wamekamilika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwa uchache wa muda wako niseme kwamba, *programmes* hizi huwa haziko *specific* ila ziko *general*. Maana yake tunaweka mafungu lakini mafungu tunayoyaweka katika bajeti hizi hayendi kwenye lile lengo tulilolikusudia, mara nyingi hutumika katika watu kufanya warsha, semina, makongamano, kufanya vitu vyengine, utakuta ni pesa nyingi lakini haziendi kwenye lile lengo tulilolikusudia.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kumshukuru sana na kumpongeza waziri pamoja na kikosi chake kazi kwa kazi nzuri sana wanazozifanya, Mwenyezi Mungu awabariki sana nashukuru.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa Wajumbe, ningewaomba sana, kwa kuwa muda inawezekana usitutoshe ningewaomba wale ambao wameleta majina hivi punde wangeandika kwa maandishi kumpelekea Mhe. Waziri. Nasema hivyo kwa sababu watu wengi wameleta maombi hapa ya kwenda kuhudhuria maziko ya Dada wa Rais wetu. Kwa hiyo sasa, wameomba na ninaona kwamba idadi ya watu itakuwa ndogo sana, hivyo ninataka niakhirishe kikao hiki saa sita kamili. Sasa wale wengine wote ambao nafikiri ni watatu tu waliobakia naomba sana wapeleke hoja zao na michango yao kwa maandishi kwa waziri. Nawashukuru.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kunipa nafasi hii kuweza kutoa mchango wangu katika Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu *(S.W)* aliyenijaalia kuwa katika uhai, uzima na afya inayoniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu. Lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza waziri husika wa wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa uwasilishaji wake mzuri ambao mimi nilipenda asimalizie asome tu. Vile vile, nimpongeze Katibu Mkuu wa ofisi hii pamoja na watendaji wote kwa shughuli yao nzuri waliyotuletea.
Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo kwa kujali muda naomba niende moja kwa moja katika mchango wangu. Mchango wangu jambo la kwanza utajikita katika mambo

haya ya utafiri. Wizara hii ina mambo ya kufanya utafiti, lakini mimi niseme tu wamefanya utafiti wa kiasi gani na baada ya kwishakufanya utafiti wanaufanyia kazi kwa kiasi gani. Kwa sababu unaweza kufanya utafiti halafu ukawa huna mafanikio yoyote kutokana na utendaji mbovu.

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu ni ya visiwa tukisema Zanzibar ni Unguja na Pemba, lakini vile vile nchi ya Zanzibar ina visiwa vidogo vidogo. Je, wamefanya utafiti ambao tunasema katika mabadiliko ya nchi huko ndiko yanakokwenda. Kuna visiwa mbali mbali na naomba ninukuu vyenye kukaliwa na watu na vyengine havikaliwi na watu, lakini vyote vina umuhimu kwa Zanzibar yetu hii.

Mhe. Mwenyekiti, kuna visiwa vidogo vidogo ambavyo vimekaliwa na watu kama vile Kisiwa cha Tumbatu, Kisiwa cha Kojani, Kisiwa cha Makoongwe Pemba, Kisiwapanza, Fundo, Uzi kwa Unguja pamoja na Mnemba kwa Unguja.

Sasa kama wanafanya utafiti wa kutosha basi tungepata yale waliyoyafanyia utafiti, lakini nasema bado hawajafanya utafiti wa kina katika sehemu yetu ya kufuatilia haya mambo ya utafiti. Ukiangalia kisiwa cha Mnemba nacho kiko hatarini katika habari ya kuzama hata katika vyombo vya habari tumesikia, lakini ni kwamba haitoshi.

Kisiwa cha Kojani hata kutembelea naona hawatembelei, lakini kwa upande wa kaskazini nacho kiko katika hali ya hatari kweli kweli. Kisiwa cha Kojani upande wa kaskazini nacho kinamegwa na maji ya bahari na inafika wakati wananchi wa Kojani upande wa kaskazini basi hawana raha hata katika shughuli zao za mapishi. Kwa sababu maji ya bahari huingia ndani ya majumba na hatima yake wanakosa hata kupika. Sisi kama wavuvi tunasema bamvua limekuwa kubwa lakini ndio hayo mabadiliko ya tabianchi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama mwakilishi wao wa Jimbo la Kojani na ni Mkojani niliyezaliwa pale, nimeanzisha ujenzi wa ukuta katika kisiwa kile unaotoka sehemu ya Ngazini mpaka ya Nkukiani, lakini sijafanikiwa kumaliza. Naiomba serikali ifanye huo utafiti wake na ikaangalie vile kulivyo na watoe msaada wao kuhusu Kisiwa cha Kojani kwa kukubaliana na haya mambo yanayotukabili. Hilo moja.

Jambo la pili nizungumzie habari ya mazingira, mazingira ina maana pana, kuna mazingira ya baharini, kuna mazingira ya nchi kavu, kuna mazingira ya kila sehemu, lakini mimi niseme katika haya mambo ya mazingira, mazingira haya tuangalie sehemu za masoko yetu yako vipi. Vile vile, tuangalie mazingira haya katika sehemu za fukwe mazingira yako vipi, lakini tukisema katika baadhi ya masoko ni sehemu ya mkusanyiko wa watu wengi ambao wanajikusanya kwa

kufanya shughuli zao, lakini ukiangalia mazingira sio mazuri. Tunaomba watu wafanye mambo kwa kuangalia mazingira yetu jinsi yanavyokwenda.

Pia, humo katika masoko inatakiwa tuwe na afya nzuri kwa mambo ya usafi, lakini bado ukiangalia nchi yetu haiko katika hali nzuri ya usafi wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, pita katika miji, natoa mfano wa hapo Michenzani katika majumba makubwa ukienda karo zote zimeziba na uchafu unatoka katika sehemu nzuri ambazo watu wanatembea na wanakusanyika kufanya shughuli zao, harufu mbaya inatoka. Lakini nasema katika hili basi ni kuwashajihisha wananchi wote pamoja na kuwa Manispaa inafanya kazi zake, lakini haiwezi kudhibiti eneo la mazingira kwa habari ya usafi ikaachiwa Manispaa pekee. Kama kweli tumekusudia kufanya mazingira ya usafi basi wananchi washiriki kikamilifu ndani ya mitaa yetu tufanye usafi na hili linawezekana, lakini naona utakuta sehemu barabara ni safi, lakini ukiingia ndani ya mitaa ni kuchafu kweli kweli hii haipendezi.

Mazingira hayo hayo serikali isimamie vizuri katika mambo ya miundombinu, tunawapa watu *tender* ya kujenga barabara wanaambiwa chimba mita mbili kwenda chini lakini wanafika mpaka mita tatu na nusu au tano wanazua maji chumvi. Mimi kwa ushahidi kamili kule sehemu ya Jimbo la Micheweni kwa Mhe. Subeit Khamis Faki, basi wamechimba mpaka maji chumvi yamejitokeza na huu ni uchafuzi wa mazingira.

Kwa hivyo, serikali katika mambo haya ya miundombinu nayo isimamie vizuri, bila ya hivyo tutakuta nchi yetu iko katika hali mbaya sana. Halafu tunasema watu wakishafanya katika uchimbaji huo wa shughuli za miundombinu basi wafanye kufukia na kupanda miti hilo halifanyiki, kama tumekusudia kweli kufanya kazi lazima haya tuyasimamie.

Vile vile, katika mambo ya mazingira kuna mambo ya vinyesi yanakwenda ovyo, mikojo utakuta sehemu watu wanajibanza tu wanakojoa sehemu ambayo haistahiki kukojoa katika sehemu ile. Haya ndio mambo ya kusimamia ili nchi yetu iwe na mazingira safi. Vile vile, katika sehemu nyengine mizoga inatupwa ovyo inaharibu mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, katika mambo hayo tukiangalia hivyo basi mimi natoa pendekezo kuwe na siku maalum ya kitaifa ukiachana na ile siku ya usafi duniani, kuwe na siku maalum ya kitaifa ya nchi yetu na iwe endelevu isiwe siku moja tunafanya usafi baadae tukaachia. Hii itakuwa ni nzuri na tutakuta mji wetu kila siku uko safi.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika mabadiliko ya nchi. Mabadiliko ya tabianchi yanakuja kama majanga na yako nje ya uwezo wetu ni Mwenyezi Mungu pekee anayeyaweza. Lakini na sisi tunafanya kama kinga na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie tuwe hivyo. Lakini mabadiliko ya tabianchi yamesababishwa na mambo mbali mbali katika dunia; ukiangalia mafuta haya watu wamekuwa wengi katika matumizi ya mafuta na ni nishati ambayo hatuwezi kuiacha, lakini kama kwamba haitoshi hata mkaa watu wanatumia kwa ajili ya shughuli zao za kila siku na miti inakatwa ovyo na sisi hatupandi miti. Hii ni hali mbaya, hivyo mabadiliko ya tabianchi yakija yanachukua sehemu kubwa katika mambo haya.

Vile vile, watu wanajikatia kuni ovyo na miti hatuipandi na mambo haya hayawezi kufikika kwa sababu siku zote watu wanaendelea na shughuli zao, lazima watu wapate kuni kwa kupikia hawawezi kutumia gesi watu wote, lakini utaratibu gani tunatumia ili nchi yetu iwe salama? Hilo ndilo la kujiuliza.

Mhe. Mwenyekiti, halafu kuna biashara chakavu zinazoletwa katika nchi yetu pia zinachangia, utakuta hapa Zanzibar imekuwa ni chaka la kuletwa mambo ya *used* ambayo mengine hayafai hata kidogo ni machaka tu, haya nayo yanachangia. Kwa hivyo, tujitahidi katika kukabiliana nayo mambo haya na kama Mheshimiwa alivyozungumza tunachukua kodi lakini mambo mengine kodi zake zinatuzuru zinatuletea majanga kuliko hiyo faida yenyewe.

Nikitoka hapo niende kwenye watu wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu kama tunavyojua hakuna hata mmoja anayependa kuwa mlemavu, lakini Mwenyezi Mungu akishakujaalia kuwa mlemavu huna jinsi, tufanye nini katika walemavu. Jambo la kwanza hawa ni kuwaonea huruma, tuwe na huruma nao walemavu, hakuna hata mmoja anayependa lakini ukishafika uwezo wa Mwenyezi Mungu lazima tukubaliane nao.

Sasa jiangalie wewe mwenyewe tu unapopata matatizo madogo unajisikia vipi halafu leo mlemavu unamkandamiza unakusudia nini. Mheshimiwa, hawa wawe na upendeleo maalum katika mambo ya afya na katika mambo ya ajira, hata katika nafasi za kugombea shughuli za uongozi basi kuwe na upendeleo hawa ni wanyonge, tusiwadhalilishe, tuwaonee huruma na tukioneana huruma na Mwenyezi Mungu anatupa mambo mazuri ya kuthaminiana, lakini bikhairi ya hivyo basi tutakuwa pabaya. Hata kwenye ajira hawa tuwape upendeleo, kuna walemavu wengine wanaweza kufanya kazi, tuwaangalie katika mambo ya ajira hawa, tukiwaangalia katika mambo hayo na wao watajisikia kama wako duniani, lakini sio anakuwa mlemavu halafu tunamkomaza zaidi, tunamdumaza, haipendezi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika sehemu nyengine niende katika udhibiti wa matumizi ya biashara haramu ya madawa ya kulevya. Hili limekuwa gumzo kubwa na linasimamiwa lakini bado haitoshi kabisa. Madawa ya kulevya yanatuathiri katika nchi yetu kupoteza nguvu kazi ya vijana. Tunao watu wetu tunaita mateja, hawa mateja ndio wanaofanya na mambo ya kuambukizana UKIMWI. UKIMWI unaupata kwa njia tofauti ikiwemo kudunga sindano na mambo mengine ya kujamiiana, lakini sio kwamba unapatikana kwa kujamiiana tu, mpaka mambo ya kudungana sindano.

Sasa leo tunakuwa kama walivyosema ni masuala mtambuka haya, vikosi vipo kila sehemu lakini suala hili siku hadi siku linazidi kukua, kwa nini? Tujiulize. Mbona tulipokwenda katika magendo ya karafuu tumeweza, kwa nini tuweze? Kwa sababu tumejikita na tumedhibiti vizuri na hili tukilisimamia vizuri serikali haiwezi kushindwa hata siku moja, bali wenyewe hatujawa tayari tu.

Kama haitoshi katika mambo haya elimu inatolewa lakini izidi kutolewa ni jambo muhimu sana, wengine wanafahamu na wengine waliobaki watafahamu, elimu ya ziada ifanywe. Lakini vile vile katika jambo hili adhabu iwe kali anayepatikana na jambo hili, bila ya kutoa adhabu kali basi kila siku itakuwa tunajirejea pale pale hatufiki.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika kinga dhini ya UKIMWI, la kuzingatia katika kinga dhidi ya UKIMWI, jambo la kwanza elimu. Elimu inatolewa siku hadi siku lakini iendelee kutolewa kwa umakini kabisa ili wapate elimu, lakini tuzingatie mambo haya yanayosababisha mambo ya UKIMWI ni sehemu nyengine katika majumba yetu ya starehe, kuwe na udhibiti na utaratibu mzuri uliowekwa. Leo mtu utamsikia dada poa na mama poa, ndio huko yanakopatikana, mtu anajali fedha tu, hajui huyu ana athari gani au vipi, watu wanachukuana ovyo ovyo tu katika majumba ya starehe. Kwa hivyo, tuweke utaratibu mzuri katika majumba ya starehe.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana nami naomba niishie hapo kwa kujali muda wako na wenzangu wanataka kutoa mchango wao. Lakini tuzingatie sana haya mambo, isiwe tunaandika kwenye vitabu mambo mazuri lakini ikawa hatuyafanyii kazi, tutakuwa tunatwanga maji katika kinu hayakai, lazima tuyasimamie vizuri hayo tunayozungumza na isiwe tunazungumza tu ikawa hayana maana yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**Mhe. Viwe Khamis Abdalla:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kuchangia machache Hotuba ya Bajeti ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii nimpongeze Mhe. Waziri kwa utendaji wake mzuri pamoja na watendaji wake wote.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na mchango wangu kwenye ukurasa wa 26 Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa dawa za kulevya. Mhe. Mwenyekiti, tume hii imefanyakazi kubwa sana ya kutoa elimu ya kuwahamasisha wananchi vijana, kutokana na janga hili la taifa lililoingia kwenye nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, janga hili la madawa ya kulevya ni janga kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, janga hili linatupotezea vijana wetu wengi, wengi wanaoathirika ni vijana. Vijana wa Zanzibar wengi wamepoteza muelekeo kutokana na janga hili la madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, kuna hizi Shehia 39 za Unguja na Pemba ambazo zimepatiwa mafunzo haya ya madawa ya kulevya. Lakini mimi kama kijana niseme kama bado tatizo hili lipo na linaendelea siku hadi siku. Kuna watu ambao wanajiona kuwa wana pesa wanafanya biashara hii ya madawa ya kulevya na serikali bado wanawalinda. Nasema hivyo makusudi kwamba serikali bado wanawalinda, kwa sababu serikali inapotaka jambo lake haishindwi. (*Makofi*)

Mhe. Bikame Yussuf Hamad amesema magendo ya karafuu serikali wameyadhibiti na kweli yameondoka. Mimi mwenyewe niko kwenye Wizara ya Fedha kwenye kamati yangu inayoshughulikia suala la karafuu. Juzi tu tuliwauliza wamesema mpaka sasa hivi kwa mwaka huu uliomaliza wa zao la karafuu hakuna mtu hata mmoja aliekamatwa na magendo ya karafuu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa nini watu hawa wanaosafirisha madawa ya kulevya wanaotuletea hapa nchini kwetu wanaowapoteza akili vijana wetu bado serikali wanawalinda.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka nilipokuwa kwenye kamati yangu ya Habari na Uwezeshaji tuliwatembelea hawa vijana walioko kwenye *Sober house*. Vijana hawa walileta malalamiko yao mengi, walisema baada ya kwisha kupatiwa yale mafunzo pale wanarudi mitaani, wanaporudia mitaani hawana kazi za kufanya. Kwa maana hiyo Mhe. Mwenyekiti, wanarudia yale yale madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, kuna hili jengo linalojengwa Dole, lakini baada ya vijana hawa wakishakutoka kwenye mafunzo hayo ya *Sober house* wanarudi mitaani. Je, serikali wamejipanga vipi kuwasaidia hawa vijana wakati wakimaliza mafunzo haya na kurudi mitaani. Mhe. Waziri namuomba atakapokuja kwenye majumuisho yake aje anieleze.

Mhe. Mwenyekiti, vijana hawa hawa ambao kuwa ndio wanaotumia madawa ya kulevya ndio wanaopata maambukizo ya Ukimwi, serikali wanatwambia kwamba sijui sindano salama. Hata hizi sindano salama ambazo utawapatia baadae na wao wana *share* na wale wenzao kwa maana hiyo maambukizo lazima wanayapata.

Mhe. Spika, nikitoka ninde kwenye uchafuzi wa mazingira. Uchaguzi wa mazingira upo na Zanzibar hauondoki, kwa sababu sisi wananchi wenyewe ndio tunaosababisha uchafuzi huu wa mazingira tutakaa tutailaumu serikali, kwa mfano wewe unapita barabarani umeshakunywa maji chupa lile la maji unalitupa pale pale njiani.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu uchafuzi huu wa mazingira mambo haya ya kukata miti. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri wizara yake washirikiane na Wizara ya Kilimo ili kuweza kulitatua janga hili linalotumiwa na misumeno ya moto. Msumeno wa moto umekuwa ni kikwazo kikubwa, miti inakatwa ovyo ovyo, hali ya hewa inapungua. Nimuombe Mhe. Waziri ashirikiane na Wizara ya Kilimo kwa sababu wao ndio wanaotoa kibali cha kukata hii miti.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye watu wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu ni muhimu sana katika nchi yetu. Watu hawa tunapaswa kuwaenzi na niipongeze wizara kwa jitihada zake zote wanazozichukuwa kuwashukughulikia watu hawa wenye ulemavu.

Niwaombe wazazi Mhe. Mwenyekiti, wawache kuwaficha vijana wao ambao kuwa wana matatizo ya ulemavu, kuna wazazi mtu akeshakumzaa mtu mwenye ulemavu mtoto yule anamficha, hampi huduma yoyote yaani anamdharau hasa kwa nini nimezaa mtoto mlemavu. Mtoto mlemavu na yeye ni mtoto kama mwengine ambaye si mlemavu. Tusiwanyanyapae, tuwaenzi kama tunavyowaenzi wengine.

Mhe. Spika, Mhe. Amina Idd alichangia hapa akasema Wizara ya Elimu watoe taaluma au elimu ya madawa ya kulevya na mimi kama Mheshimiwa ninatoka kwenye vijana naunga mkono elimu hii itolewe mashuleni, ili vijana wetu waweze kuijua athari ya madawa ya kulevya tokea bado wako shuleni. Madawa ya kulevya Mhe. Mwenyekiti, yanakusababisha mpaka unakwenda kwenye ubakaji, ukitembea usiku maeneo ya Jang'ombe una wasi wasi, unaweza ukatolewa roho yako kwa shilingi mia tano au simu ya shilingi elfu thalathini. Hili ni janga kubwa sana serikali waliangalie kwa umakini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango huo naunga mkono bajeti hii ya Mhe. Waziri asilimia mia moja. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe sasa nimuombe Mwanasheria Mkuu aweze kutengua Kanuni ili basi tuweze kutoka mapema saa 6:00 na kuweza kuhudhuria katika maziko ya Mhe. Rais wetu.

Kabla ya hapo nimuombe Mhe. Zahra Ali Hamad nafikiri alikuwa na majibu kutoka kwa masuala mbali mbali ya Wajumbe kutoka wizara yake, nimuombe amalizie hilo baada ya kurudi jioni baada ya hapo yatafuata majumuisho ya Mhe. Waziri. Mhe. Mwanasheria Mkuu karibu. (*Makofi*)

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo tunafahamu kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amefiliwa na dada yake na wengi wa Wajumbe wako Mhe. Mwenyekiti wanataka kwenda na kuungana nae Mhe. Rais katika maziko ambayo tunataraja yafanyike saa 7:00 adhuhuri. Kwa mnasaba huo Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe hoja ya kuahirisha kikao hiki cha Baraza hadi saa 11:00 jioni hii ya leo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Afya na ustawi wa Jamii:** Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo sasa naakhirisha kikao hichi hadi saa 11:00 barabara jioni.

*(Saa 5:50 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)*

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninaunga mkono hoja. Mhe. Mwenyekiti, wachangiaji ambao walichangia kuna masuala mawili matatu yanayohusu Wizara ya Elimu na

Mafunzo ya Amali. Kwa hivyo, nimehisi ni vyema nimsaidia Mhe. Waziri kabla ya kufanya majumuisho yake.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad yeye alitaka kujua ni wanafunzi wangapi au ni vijana wangapi wenye ulemavu ambao Bodi yetu ya Mikopo ya Elimu ya Juu imewapatia nafasi.

Mhe. Mwenyekiti, walemavu wana milango tofauti ya kupata mikopo hii. Mlango wa kwanza wa kupata mikopo hii kupitia Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, na pale huwaandikiwa barua ya kuthibitishiwa kwao na wao wenyewe huipeleka kwenye Bodi yetu ya Mikopo.

Lakini wa pili hupitia Jumuiya ya Watu Ulemavu na pale hupewa barua ya kuthibitisha ulemavu wao na Bodi yetu huwapatia mkopo. Lakini mlango wa tatu ni mtu mwenyewe binafsi kwa kupitia utaratibu wa Bodi yetu ya Mikopo uliowekwa kuomba na sisi tukibaini tukijua kama huyo ni mlemavu, kwa sababu ulemavu mara nyingi Mhe. Mwenyekiti, unakuwa haufichiki, hutoa kipa umbele kwa mtu huyo.

Na kwa kuelewa umuhimu wa kuwaendeleza ndugu zetu wenye ulemavu katika masomo ya elimu ya juu, Bodi ya Mikopo huzingatia mahitaji ya makundi haya yenye mahitaji maalum Mhe. Mwenyekiti.

Bodi ikipata tu *admission letter* kutoka chuo husika ambacho ameomba basi kijana huyu huwa tunampatia mkopo. Kama tunavyojua Mhe. Mwenyekiti, Serikali imeweka vipa umbele kwa Bodi yetu ya Mikopo. Kuna vipa umbele vile ambavyo ndiyo mahitaji ya nchi, vile ndivyo ambavyo tunavitazama kwanza katika kuwapatia mikopo vijana wetu.

Kwa upande wa wenzetu walemavu bila ya kuzingatia vipa umbele hivyo, kwa mfano *business administration* karibu miaka hivi sasa hatutoi mikopo. Lakini ikiwa ni mwenzetu mwenye ulemavu basi sisi hatutizami vile vipa umbele vya Serikali, moja kwa moja kijana huyo humpatia mkopo.

Pia, kwa kuthamini kundi hili katika Sheria yetu ya Bodi ya Mikopo ambayo tuliipitisha hapa kwenye Kifungu cha 4(1) katika kuunda Bodi ya Wakurugenzi. Kifungu hiki kimetoa nafasi moja ya mwakilishi wa kundi hili. Kwa hivi sasa ni Ndugu yetu Abdulwakil Haji ndiye ambaye anawakilisha katika Bodi ya Mikopo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohammed Mbwana Hamad alitaka kujua kama ni wanafunzi wangapi ambao hivi sasa tumewapatia mikopo na wapo chuoni. Mikopo ambao tumewapatia mikopo na wapo chuoni ni wanafunzi saba. Mmoja ana

ulemavu wa *albino*, yupo Chuo cha Uganda mwengine *albino* hivyo hivyo yupo Chuo cha Chukwani na mmoja yupo *UDOM* mlemavu wa viungo. Hii ulemavu wa viungo Zanzibar University Uziwi, *SUZA* yupo mwengine tena mmoja uziwi na Chuo Kikuu Huria ulemavu wa kiungo pia yupo mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, pia kulikuwa na suala jengine ambalo lilijitokeza la Mhe. Subeit Khamis Fak ambaye yeye alitaka kujua kuwa wanafunzi tunawachanganya pamoja katika madarasa maalum ya mjumuisho wakiwa wakiwemo wasiona, viziwi, wenye ulemavu wa akili. Lakini mbona walimu hawatumii lugha ya alama.

Mhe. Mwenyekiti, walimu wote wa skuli ambazo zimeteuliwa na kuingiziwa *programme* ya elimu mjumuisho hupewa mafunzo maalum ambayo wanamudu na kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Aidha, wanafunzi wasioona kwa mfano wao hufundishwa kwa kupitia nukta nundu. Hupatiwa mashine ya *Braille* ambayo pia hupewa na kazi zake za kuandikia. Mafunzo haya huwa wanapatiwa walimu pamoja na wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano mwaka 2012/2014, walimu 136 wa Unguja na Pemba walipatiwa mafunzo ya nukta nundu na wanafunzi 66 walipatiwa mafunzo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, pia, kwa wanafunzi viziwi, walimu wanaofundisha hupewa mafunzo ya lugha ya alama, ili waweze kufahamiana katika kufundisha. Vile vile wanafunzi hawa hupatiwa wanafunzi wenziwao wawili ambao wanakuwa ni marafiki zao kwa kuweza kuwasaidia.

Vile vile, walimu pia tumewapatia mafunzo lakini na wanafunzi wenyewe wenye uziwi tunawapatia mafunzo, lakini pia na wale marafiki zao wawili pia huwapatia mafunzo. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka 2012/2014 walimu 102 tuliwapatia mafunzo ya lugha ya alama. Wanafunzi 126 pia walipatiwa mafunzo hayo lakini na wale wanafunzi wenziwao; marafiki zao wale 246 tuliwapatia mafunzo ya kuweza kuwasaidia wenziwao wakiwa ndani ya darasa au nje ya darasa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hali hii kwa kiasi fulani wanafunzi wanaweza ku-*cope* na wenziwao kama wanafunzi wa kawaida. Mhe. Mwenyekiti, licha ya mafanikio hayo ninataka nikiri kama bado tuna changamoto, kwa sababu Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Amali hatujaweza kufikia wanafunzi wote ambao wana mahitaji maalum. Skuli ambazo zimefikia ni 135 tu na skuli zetu kwa jumla ni 450.

Kwa hivyo, utaona kama kuna skuli karibu mia tatu naa ambazo hatujawafikia wanafunzi ambao wana mahitaji maalum. Hivyo Mhe. Mwenyekiti, ninalotaka kusema kama bado tuna changamoto na tutajihidi kadri ambavyo bajeti itaturuhusu ili kuweza kufikia na hizi skuli nyengine ambazo kuna wanafunzi wenye mahitaji maalum ili waweze kupata elimu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba kuunga mkono hoja. Ninakushukuru sana. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo na Amali kwa ufafanuzi wako mzuri. Sasa hivi tunampa nafasi basi Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa ajili ya kujibu hoja za Wajumbe kama zilivyoulizwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais**: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya njema na kunipa mimi uwezo wa kusimama tena mbele ya Baraza lako hili tukufu, kwa ajili ya kufanya majumuisho na kutoa ufafanuzi wa hoja ambazo zilizochangiwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, kabla ya yote naomba uniruhusu nichukue nafasi hii kutoa mkono wa pole kwa Kiongozi wetu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa msiba uliowafika yeye na familia yake ya kuondokewa na dada yao mpendwa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu pahala pema na kuwajaalia subra kubwa wafiwa katika kipindi hiki.

Mhe. Mwenyekiti, ninachukua fursa hii adhimu kuendelea kumshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kuendelea kunikubali katika nafasi hii ya kumsaidia kutekeleza majukumu ya Ofisi yake na kuendelea kutupa miongozo na ushauri wake wa busara katika kipindi chote, mimi na watendaji wangu tokea kuanzishwa kwa Ofisi hii ya Makamu wa Makamu wa Kwanza wa Rais chini ya Serikali yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee ninapenda pia kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini kulitumikia taifa katika nafasi hii na kwa miongozo yenye hekma na busara wakati wote wa kutekeleza majukumu yao. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee ninapenda sasa kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako hili waliopata fursa ya kuichangia kwa kuzungumza au kwa maandishi hotuba yetu, kwa mwaka huu wa fedha 2015/2016 ambayo ni ya kwanza katika kutumia mfumo huu wa *PBB.*

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba michango yote waliyoitoa tunaithamini sana na kwa imani kwamba lengo lao lilikuwa ni kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yetu kupitia malengo tuliyojiwekea, ili hatimaye kuweza kufikia utoaji wa huduma tunaokusudia.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutoa ufafanuzi wa hoja zilizotolewa naomba nikiri kwamba sitoweza kuizungumzia kila hoja kwani ni nyingi. Kwa hivyo michango yote iliyotolewa katika hali ya mapendekezo, ushauri, miongozo na maelekezo, ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu watuamini kuwa tumeipokea na ninapenda kuwahakikishia kwamba tutaifanyia kazi kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyojaalia.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa ufafanuzi wa hoja zilizotolewa, naomba nichukue fursa hii kuwatambua Wajumbe wale ambao wamechangia kwa kuzungumza ndani ya Baraza hili, nao ni 20. Lakini kuwatambua ambao wamechangia kwa maandishi ambao ni 4.

Waliochangia kwa njia ya mazungumzo ndani ya Baraza hili, nao ni:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
3. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
4. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
5. Mhe. Subeit Khamis Faki
6. Mhe. Salim Abdalla Hamad
7. Mhe. Mgeni Hassan Juma
8. Mhe. Abdi Mosi Kombo
9. Mhe. Fatma Mbarouk Said
10. Mhe.Mahmoud Muhammed Mussa
11. Mhe. Mohammed Haji Khalid
12. Mhe. Rufai Said Rufai
13. Mhe. Mussa Ali Hassan
14. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
15. Mhe. Ashura Sharif Ali
16. Mhe. Amina Iddi Mbarouk
17. Mhe. Omar Ali Shehe
18. Mhe. Hassan Hamad Omar
19. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
20. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

Ninamshukuru sana Mhe. Zahra Ali Hamad ambaye ni Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa ufafanuzi wake juu ya masuala ya watu wenye ulemavu na elimu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni:-

1. Mhe. Salma Mussa Bilal
2. Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
3. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
4. Mhe. Marina Joel Thomas

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo na kuweza kuwatambua majina Waheshimiwa Wajumbe waliopata nafasi ya kuchangia hotuba yetu, sasa naomba kutoa ufafanuzi wa masuala ya jumla. Na nitaanza kwa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kama walivyochangia Waheshimiwa Wajumbe wote kuwa Zanzibar inakabiliwa na athari kubwa zinazoambatana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Maeneo mbali mbali yakiwemo ya kilimo Unguja na Pemba yameathiriwa na suala hili na kuwafanya wananchi maeneo hayo kutoweza kuendelea shughuli zao za kilimo ipasavyo.

Aidha, sehemu mbali mbali za ukanda wa pwani Unguja na Pemba hasa zile ambazo zenye fukwe za mchanga zimeathiriwa na mmomonyoko. Kwa kuwa Zanzibar ni visiwa ni dhahiri kuwa shughuli zote kuu za kiuchumi zinaathiriwa na suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kulitambua hilo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na wadau mbali mbali imetayarisha na kuzindua mkakati wa mabadiliko ya tabianchi Zanzibar. Kwa ajili ya utekelezaji wa mkakati hiyo, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, hivi sasa inaandaa mpango kazi ambao unategemewa kumalizika mwezi wa Januari, 2016 kwa hatua za uhamasishaji wa nyenzo za utekelezaji.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mpango kazi huo utatoa kipaumbele cha maeneo ya utekelezaji hatua kwa hatua kwa mujibu wa upatikanaji wa fedha utakavyokuwa.

Mhe. Mwenyekiti, Uharibifu na Uchafuzi wa Mazingira. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa Zanzibar inashuhudia uharibifu na uchafuzi mkubwa wa mazingira ambao udhibiti wake unahitaji msukumo mkubwa wa kisheria na kitaasisi. Kutokana na hali hiyo, ndiyo maana Serikali imetayarisha Sheria mpya ya Mazingira na pia kuweza kuunda Taasisi mahususi ya uzingatiaji na usimamizi wa sheria hiyo.

Ni imani ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuwa Waheshimiwa Wawakilishi, taasisi za kiserikali, binafsi, jumuiya za hiyari na jamii kwa jumla watatoa mashirikiano yao katika kuhakikisha kuwa sheria na taasisi hiyo inafanya kazi ipasavyo, ili kupunguza uharibifu na uchafuzi wa mazingira katika visiwa vyetu vya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, aidha Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais itaendelea kutoa elimu ya mazingira kwa jamii na wadau mbali mbali, ili kuhakikisha kuwa kuna ushiriki mzuri kwa kila mmoja wetu katika kulinda na kuhifadhi mazingira yanayomzunguka.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa ufafanuzi wa maeneo hayo makuu ambayo yalichangiwa na Waheshimiwa Wajumbe wote, sasa kwa ruhusa yako napenda kutoa ufafanuzi wa maeneo maalum kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia napenda kuishukuru sana hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kwa uchambuzi iliyoufanya ambao naamini umewapa uelewa zaidi Waheshimiwa Wajumbe, juu ya malengo ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Aidha, nakubaliana na hotuba hiyo ya kamati juu ya suala zima la uhaba wa fedha, kwa ajili ya kupambana na tatizo la dawa za kulevya nchini, pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi, ambazo kwa kiasi kikubwa zimeathiri maeneo mengi kisiwani Pemba. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais itaendelea kuyatizama masuala haya, pamoja na mengine kwa umuhimu wa aina yake.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya ufafanuzi huo wa jumla na kwa michango iliyotolewa, naomba sasa kufanya majumuisho ambayo nitayagawa katika maeneo makuu manne kama haya yafuatayo:

1. Mazingira na mabadiliko ya tabianchi
2. Masuala ya watu wenye ulemavu
3. Masuala ya dawa za kulevya
4. Masuala ya ukimwi

Kuhusu masuala ya mazingira. Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inayotaarifa ya uchimbaji wa mchanga katika eneo la Giningi kisiwani Pemba. Ni lazima tukubali kwamba katika shughuli zetu mbali mbali za kimaendeleo, bado tunahitaji maliasili hiyo ya mchanga. Kutokana na umuhimu huo serikali imetenga maeneo rasmi kwa ajili ya uchimbaji na uchukuaji wa mchanga, na eneo la Giningi ni moja kati ya maeneo hayo. *(Makofi)*

Aidha, miongozo ya uchimbaji mchanga na mikataba ya uendelezaji wa eneo hilo baada ya uchimbaji imetolewa kwa wadau hao. Mhe. Mwenyekiti, ni imani ya ofisi yetu kwamba eneo hilo litaimarishwa baada ya shughuli za uchimbaji kukamilika. Aidha, ofisi yetu inaahidi kuendelea kuwa karibu na kuweza kutoa elimu ya mazingira katika eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye kitabu changu cha hotuba, kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar ameshaisaini sheria mpya ya mazingira, na kwa bahati nzuri Mhe. Rais siku ya Ijumaa tarehe 22 Mei, 2015 amemteuwa rasmi Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, ambaye ni ndugu Sheha Mjaja Juma. *(Makofi)*

Aidha, nafasi aliyoiwacha wazi ya Mkurugenzi wa Mazingira, ameteuliwa ndugu Juma Bakar Alawi kuweza kuongoza idara hiyo. Nachukuwa fursa hii kuwapongeza Wakurugenzi hao, na kuwatakia kazi njema katika kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, tunakubaliana na hoja ya uendelezaji wa maeneo ya machimbo, hasa kwa kuwa imezingatiwa katika sheria mpya ya mazingira. Tunaahidi kuwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, itaisimamia sheria hiyo kikamilifu ili kuhakikisha kuwa maeneo ya machimbo yanaendelezwa baada ya shughuli za uchimbaji.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuliarifu Baraza lako kuwa serikali kwa kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili, imeweka siku ya tarehe 14 Aprili ya kila mwaka, kuwa ni siku ya upandaji miti kitaifa. Siku hiyo imeanza kutekelezwa toka mwaka 2011. Miti mbali mbali ya matunda na mengineyo imekuwa ikipandwa kwa ajili ya kuadhimisha siku hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako na wananchi kwa jumla, kutumia siku hiyo kupanda miti hasa ya matunda katika maeneo yao, ili kukifanya Kisiwa cha Zanzibar kuendelea kuwa kisiwa cha kijani.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, inakiri kuwa Kisiwa cha Mtambwe Mkuu kama yalivyo maeneo mengi ya Zanzibar, kinaathirika kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Juhudi mbali mbali zimechukuliwa katika eneo hilo zikiwemo za utoaji wa elimu ya mazingira pamoja na upandaji wa miti.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi yetu inaahidi kulichukulia suala la uwandani kwa kuwasiliana tena na wizara husika, kwa ajili ya wizara hizo kutumia fursa zilizopo ili kuvipatia vikundi vya ushirika vilivyoundwa katika eneo hilo njia mbadala ya

kujikimu kimaisha, ili waweze kuachana na shughuli za uchimbaji wa matofali, ambazo zinaleta athari kubwa za kiafya na za kimazingira.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa kisiwa cha Mnemba ni moja ya maeneo yaliyoathiriwa kwa kiwango kikubwa na mmomonyoko wa fukwe. Ofisi yetu kwa kupitia Idara ya Mazingira kwa kushirikiana na wajumbe wa Kamati ya kitaalamu ya usimamizi wenye uwiano wa kanda ya pwani, wamefanya ziara mara mbili kwa ajili ya kuona hali halisi ya kisiwa hicho. Katika ziara hiyo ushauri na miongozo mbali mbali imetolewa ambayo inaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, ofisi yetu inaahidi kuendelea kufuatilia kwa karibu maendeleo ya kisiwa hicho.

Masuala ya watu wenye ulemavu. Mhe. Mwenyekiti, watu wenye ulemavu waliopatiwa visaidizi Unguja na Pemba ni watu 225 na utaratibu uliotumika ilikuwa ni kufanya uhakiki kwa kila wilaya, ili kutambua mahitaji halisi kisha kuvigawa visaidizi kwa mujibu wa mahitaji. Hata hivyo, utaratibu huo haukufanyika kwa kuzingatia mgawanyo wa majimbo.

Mhe. Mwenyekiti, misaada ya kawaida wanayopatiwa watu wenye ulemavu mpaka hivi sasa, ni ruzuku kwa ajili ya kupitia Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu, ambazo ni shilingi milioni 1,800,000 kwa kila Jumuiya.

Aidha, ofisi yetu inatoa ushauri na maelekezo katika kufuatilia mambo tofauti yanayowakabili watu wenye ulemavu, pamoja na kuwapatia mafunzo ya *study* za maisha. Kwa upande wa msaada wa kujiendeleza kielimu, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inawasiliana na Bodi ya Mikopo kama Mhe. Naibu Waziri alivyoeleza, ili kuwapa kipaumbele watu wenye ulemavu. Vijana 30 wameombewa kupatiwa mikopo kupitia Idara ya Watu Wenye Ulemavu kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza na Shahada ya Pili.

Mhe. Mwenyekiti, watu wasioona wanajifunza kwa maandishi ya nukta nundu *braille* na pia hutumia programu maalum za *jaws* kwa kutumia *Laptop,* viziwi wanajifunza kwa kutumia lugha ya alama na hivyo kutakiwa kuwepo wakalimani.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya shilingi milioni 167,546,569 ziliweza kukusanywa kwa ajili ya mfuko wa maendeleo ya watu wenye ulemavu. Mfuko wa Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu, upo kwa mujibu wa sheria ya watu wenye ulemavu ya haki na fursa sawa namba 9 ya mwaka 2006, kifungu cha 38 na kwa manufaa ya watu wenye ulemavu.

Matumizi ya fedha za mfuko wa watu wenye ulemavu yatafanywa na Baraza la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar na Mfuko huu unategemewa kuwa endelevu.

Vianzio mbali mbali ikiwemo asilimia 25 ya kodi ya miundombinu ambayo itagaiwa katika mifuko mitano ambayo tunayo.

Kwa hivyo, *source* moja ya *fund* ya mfuko huu itatokana na kodi ile ya mfuko wa miundombinu, ambao utatoa asilimia 25 na itagaiwa katika mifuko mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu sheria ya watu wenye ulemavu, tayari iko katika mpango wa kufanyiwa mapitio ili kuona kwamba inakidhi haja. Hata hivyo, mapitio hayo yanasubiri kukamilika kwa sera ya watu wenye ulemavu ambapo hivi sasa ofisi yetu inakamilisha taratibu ya kuiwasilisha serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, tumepokea ushauri wa Mhe. Mshimba alioutoa juu ya visaidizi hasa *wheelchairs*, yaani viti vya magurudumu mawili ambavyo vitakuwa ni rahisi kutumiwa na watu wenye ulemavu wa viungo, kwani vitatumia umeme au *electronic*.

Hata hivyo, vigari vya umeme ni ghali ukilinganisha na fedha tuliyonayo. Pia kutokana na mazingira yetu ni vyema tukaanzia na hivyo vya kawaida, hasa ukizingatia barabara zetu hazina mazingira rafiki na mazuri kwa ajili ya kutumia vitu hivyo, ukilinganisha na nchi nyengine duniani.

Masuala ya Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Mhe. Mwenyekiti, tume imeona umuhimu wa kushirikiana na jamii na hivi sasa tume imezindua mpango wa kufanya kazi pamoja na wilaya kwa kuwashirikisha viongozi wa wilaya, masheha, wakuu wa polisi wilaya, awkuu wa polisi jamii, askari shehia na vikundi vya ulinzi shirikishi vya shehia, kama vilivyoelezwa katika kitabu cha hotuba yangu.

Mhe. Mwenyekiti, serikali iko makini katika kutekeleza majukumu yake kama nilivyoeleza katika hotuba yangu. Biashara ya dawa za kulevya ni tofauti kabisa na kupambana na magendo ya karafuu, au udhibiti wa mifuko ya plastiki kama Waheshimiwa Wajumbe wanavyoona.

Biashara hii ni biashara ya kimataifa ambayo inafanywa na wenye mitaji mikubwa, ambapo nchi zilizoendelea na zenye uwezo mkubwa wa kiusalama, bado hazijafanikiwa katika kulidhibiti kwa ukamilifu suala hili.

Aidha, maumbile ya nchi yetu ni visiwa ambavyo vina bandari nyingi bubu na pia kuingia kwake inaingizwa kwa mbinu za hali ya juu. Kwa mfano, dawa za kulevya aina ya unga unaweza kusafirishwa hata kwenye betri mpya ya gari pasi na kujua tofauti ya gunia la karafuu.

Vile vile, tatizo hili linachangiwa zaidi na kuwepo kwa miundombinu duni ya kiusalama, pamoja na muhali wa kuwatolea taarifa wahusika kutokana na ukaribu wa kujuana kwetu. Hivyo, udhibiti wa tatizo hili unahitaji juhudi za pamoja za kutoa taarifa kwa utaratibu uliowekwa kwenye vyombo husika bila ya kujali uhusiano uliopo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu takwimu za kesi za dawa za kulevya, naomba nizitaje hapa kama tulivyozipokea kutoka kwenye vyombo vyetu kama ifuatavyo. Kwa mwaka 2014, kezi zote ni 80, kesi zilizo mahakamani ambazo zimesikilizwa ni 52, kesi zilizo mahakamani ambazo upelelezi unaendelea ni 11, kesi zilizofutwa ni 16, na kesi iliyopata humu ni moja tu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2015 kesi zote ni 34, zilizokuwa mahakamani ambazo zinaendelea kusikilizwa ni 12, zile ambazo upelelezi unaendelea ni 21, hakuna kesi iliyofutwa na kesi ambayo imepatiwa hukumu ni moja. Hizo ni takwimu kuhusiana na kezi za dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, ili *Sober House* ipate ruzuku inayotolewa na serikali kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, mambo yafuatayo lazima yatimizwe.

Kwanza, usajili; nyumba lazima iwe imesajiliwa kwa taratibu iliyotolewa na muongozo wa kuendesha nyumba za marekebisho ya tabia, kiutaratibu kila kiongozi wa nyumba anatakiwa aombe usajili kwa nyumba kila baada ya mwaka mmoja.

Pili, tume inatoa usajili wa nyumba husika endapo itatimiza vigezo vya miongozo ya *Sober House* katika kiwango cha chini kabisa. Sababu ya kukosa fedha katika kipindi hichi, nyumba iliyoripotiwa haikupatiwa fedha, ni kwa sababu bado *Sober House* hii haikukidhi vigezo vilivyowekwa katika muongozo kwa kiwango cha chini kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nyumba hiyo inayoripotiwa haikuomba usajili wake kwa mwaka huu kwa tume, jambo ambalo linapelekea pia kutoweza kupatiwa fedha, na katika kaguzi zinazofanywa na tume za kushtukiza, imegundulika kwamba nyumba hii ina kasoro nyingi, ambazo zinapingana na muongozo na taratibu za uendeshaji wa nyumba za marekebisho ya tabia, yaani *Sober House*.

Tume iliiandikisha nyumba hiyo zaidi ya mara tano, ikiwemo pamoja na kumwita mmiliki wa nyumba hiyo ana kwa ana, kwa lengo la kumtaka arekebishe kasoro za nyumba anayoiendesha, lakini hakuna lolote ambalo limefanyika katika nyumba hiyo. Hata hivyo, katika kaguzi zilizofanywa na tume imegundulika kwamba

nyumba hiyo sasa imeshafungwa kwa kipindi kirefu bila ya kutolewa taarifa kwa tume.

Mhe. Mwenyekiti, idadi ya vijana wanaotumia dawa za kulevya kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2012/2013 inakisiwa kuwa karibu vijana 10,000 wanatumia dawa za kulevya hapa visiwani kwetu Zanzibar. Kati ya hao wanaotumia dawa kwa njia ya kujidunga ni 3,200 na wenye maambukizo ya virusi katika hao ni asilimia 11.2 kati ya hao wanaojidunga.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wanaomaliza muda wao kwenye nyumba za marekebisho ya tabia, serikali imekuwa ikiwapatia taaluma ya kuwasaidia katika kazi za ujasiriamali. Hivi sasa tayari kuna nyumba zimesaidiwa kwa kupata miradi tofauti, kupitia kwa wadau wetu wa maendeleo *UNODC.* Miradi hiyo ni pamoja naufugaji wa ng'ombe, kuku na kazi za mikono ambazo zimekuwa zikifanywa na vijana hao. Hivi karibuni tumewakabidhi vifaa kama kompyuta na mashine za kuoshea gari, kwa ajili ya kuwawezesha vijana hao kimaisha.

Masuala ya Tume ya UKIMWI. Mhe. Mwenyekiti, hadi sasa hakuna chonjo wala dawa ya ukimwi iliyopatikana. Njia kuu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya ukimwi ni kwa watu kuweza kubadilisha tabia zao. Tabia hubadilishwa kwa watu kuweza kupeana onyo, kupeana elimu na kushauriana kupitia makongamano, mikutano, matangazo na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Ukimwi imewaandaa waelimishaji rika ndani ya makundi maalum, ambao ndio wanafanyakazi chini ya Tume ya Ukimwi katika utoaji wa elimu ya ukimwi. Waelimishaji rika hawa wameanzisha mtandao wa kuweza kuyafikia makundi maalum, yakiwemo yale tunayoyaita kwa jina la dada poa na kaka poa.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imekuwa ikiongeza ruzuku kwa Tume ya Ukimwi kwa kila mwaka kuanzia mwaka 2011/2012. Pia ofisi yetu ipo katika hatua ya mwisho katika kutayarisha waraka wa kuanzisha mfuko wa ukimwi. Zoezi hili litakapokamilika basi litapunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa fedha za nje, na badala yake kuweka mkazo katika kutenga na kutafuta fedha zinazotokana na vyanzo vya ndani.

Mhe. Mwenyekiti, kuanzia mwaka wa fedha 2007 utafiti wa kibalojia na kitabia kwa makundi maalum, ulionesha kuwa makundi ya watu wanaoishi na virusi vya ukimwi yanachochewa kwa kasi kubwa na makundi maalum, ambayo ni pamoja na wanawake wanaojiuza na wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao. Kiwango hicho ni kama ifuatavyo.

Wanaume wanaojiuza ni asilimia 10.8 na wananume wanaofanya mapenzi na wanaume wenzao ni asilimia 12.3, wakati maambukizi katika jamii yalipokuwa ni asilimia 0.6. Takwimu hizo ndizo zilizopelekea kuanzishwa program maalum kuyalenga makundi haya, ili kuweza kudhibiti maambukizi yasienee katika jamii, kwani makundi yanaingiliana kwa kiasi kikubwa na jamii. Pragramu hizo ni kuwapatia huduma za afya ambazo ni ushauri nasaha na upimaji, matibabu ya magonjwa ya kujamiana, kuwapatia rufaa na tiba, pamoja na elimu ya masuala mbali mbali ya kinga na tiba.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Ukimwi imepewa dhamana ya kuratibu mwitiko wa kitaifa wa kupambana na ukimwi unaojumuisha sekta zote. Juhudi ambazo zimechukuliwa ni kuweza kuweka miongozo kujenga uwezo, kutetea na kuweka mifumo mingine. Tume ya Ukimwi imeweka miongozo katika mkakati wa pili wa kupambana na ukimwi na vile vile sheria ya kusimamia na kukinga ukimwi, kuzijengea uwezo asasi mbali mbali na kushirikisha kwa kiwango kikubwa taasisi za kidini.

Mhe. Mwenyekiti, juhudi hizi za pamoja na taasisi mbali mbali ndizo zinazoifanya Zanzibar kuendelea kuwa na kiwango kidogo cha maambukizi kwa muda mrefu, tofauti na hali ilivyo katika nchi za Afrika ya Mashariki na Kusini mwa Bara la Afrika.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwatoa wasi wasi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kuhusu dhana ya kuongezeka kwa maambukizi ya virusi vya ukimwi. Tafiti mbili zilizofanyika nchini ambazo ndizo zinazotumika kama rejea, hazioneshi ongezeko la kasi kama ilivyofikiriwa na watu wengi. Utafiti wa mama wajawazito uliofanywa na Wizara ya Afya mwaka 2014, umeonesha kuwa kiwango cha maambukizi bado ni asilimia 0.6. Utafiti mwengine ni ule wa viashiria vya ukimwi na maleria ambao ulionesha asilimia 1.

Hata hivyo, kitaalamu hakuna ongezeko halisi kutokana na mwanya wa utafiti na kwa mujibu wa uchambuzi wa kitakwimu.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo, wizara yangu inakubali kwamba kuna ongezeko la tabia hatarishi ndani ya visiwa hivi, ambapo kila mmoja ana wajibu wa kuchukua hatua. Ofisi yetu inachukua hatua hii kuzikumbusha wizara, taasisi binafsi na wadau mbali mbali kwamba zina wajibu wa kutekeleza programu, na kuingiza masuala ya ukimwi katika kazi zao za kila siku. Jambo hili kwa sasa limezorota. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili, kusaidia katika hali hii wakati wa kuangalia utekelezaji wa shughuli za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la programu kuu na ndogo zilizomo kwenye taasisi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Namshukuru sana Mhe. Omar Ali Shehe kwa mchango wake mzuri juu ya programu hizo. Ni kweli kuwa mambo mengi ambayo Mhe. Omar Ali Shehe ameyachangia yamo kwenye matokeo yanayotegemewa kupatikana kwenye program hizo, na yale mengine ambayo hayamo katika programu za ofisi yetu, yamezingatiwa katika programu ya taasisi nyengine husika.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ukubwa wa bajeti ya utawala, umetokana na kuwepo matumizi ya mishahara katika program hizo. Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena nachukua fursa hii kuwashukuru sana wale wote waliochangia, kwani michango yao inaelekea katika kujenga na kuelekeza. Naomba niendelee sasa na ufafanuzi kidogo kuhusiana na masuala maalum.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa wa Jimbo la Kikwajuni na Mhe. Ashura Sharif Ali, walitaka kuelewa juu ya fedha za mabadiliko ya tabianchi. Kwa ujumla serikali ingependa kuchangia fedha kwenye mabadiliko ya tabianchi, lakini kutokana na ufinyu wa bajeti, fedha ziliopo ndio maana imehamasisha fedha kutoka kwa wahisani, ili ipate fursa ya kusimamia suala hili kubwa. Sambamba na hilo serikali inachangia vitendea kazi na mishahara kwa wafanyakazi wanaosimamia shughuli za mabadiliko ya tabianchi, waliopo ndani ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira.

Aidha, mpango kazi wa utekelezaji mkakati wa mabadiliko ya tabianchi utakaotayarishwa utategemea kutoa fursa kwa Serikali kuweka bajeti kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa mpango huo.

Kuhusu suala la Mheshimiwa Mahamoud kuhusu Kizingo na eneo la Kilimani na maeneo mengine ya kilimo kama nilivyochangia katika hotuba yangu kiujumla na kama ilivyoelezwa kwenye hotuba ya Afisi ya Makamu wa Pili, kuwa maeneo ya Kilimani wakati nachangia Ofisi ya Makamu wa pili maeneo ya Kilimani, Bwawani na Kisiwapanza, Ukele, Tumbe na Tovuni ni maeneo ambayo yamo katika mradi wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi yanayosimamiwa kwa pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Bikame alitaka kujua je, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ina maofisa kwenye Halmashauri ambao wanatoa vibali vya ujenzi. Mhe. Mwenyekiti, ofisi yetu kupitia Idara ya Mazingira haina maofisa kwenye halmashauri wanaotoa vibali vya ujenzi wala kisheria Idara hiyo haihusiki kutoa vibali vya ujenzi.

Hata hivyo sheria mpya ya mazingira inazitaka Taasisi na Halmashauri zote kuwa na Vitengo vya mazingira na mabadiliko ya tabia nchi ili kuweza kusaidia masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabia nchi kuweza kuingizwa katika mipango mbali mbali ya taasisi na Halmashauri hizo. Naomba nitoe wito kwa Taasisi na Halmashauri zote waweze kuanzisha vitengo hivyo, ili mipango yao ya maendeleo iweze kuzingatia uwekeji wa mazingira.

Mhe. Viwe, aliulizia suala la msumeno wa moto, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili imeshatayarisha kanuni ya kupiga marufuku kabisa sasa matumizi ya msumeno wa moto, na kwa mujibu wa kanuni hiyo matumizi ya msumeno wa moto yataruhusiwa kwa kazi maalum tu tena za dharura au maafa kanuni hiyo inategemewa kuwa tayari hivi karibuni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine tena niwashukuru wajumbe kwa kunivumilia na kuweza kunisikiliza ufafanuzi huo, naamini ufafanuzi niliotoa umeweza kuweka bayana yale yote yaliyokuwa yanahitaji maelezo ya ziada. Vile vile, naamini kuwa Waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako tukufu wataendelea kuiunga mkono Ofisi ya Bajeti yetu katika kuweza kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake kwa faida ya jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sasa naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimkiwa wajumbe wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa waliokubaliana wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais:**Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya matumizi ili liweze kuvipitisha vifungu vya matumizi vya ofisi yangu.

**KAMATI YA MATUMIZI**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **FUNGU B01** | **OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS** | | |
| Kifungu 04 | Idara ya Mazingira Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira | Sh. | 34,712,000 |
| | **Juma la ya Fungu** | **Sh.** | **34,712,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU B 01 - OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS**

| | |
|---|---|
| Makadirio ya Kazi za Kawaida | Sh. 2,923,400,000 |
| Makadirio ya Kazi za Maendeleo | Sh. 450,000,000 |
| **Jumla Kuu** | **Sh. 3,373,400,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

FUNGU B 01 - P01- PROGRAM YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA MABADILIKO YA TABIA NCHI

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu S01 | Usimamizi wa Mazingira | Sh. 174,076,000 |
| Kifungu S02 | Usimamizi wa Mabadiliko ya Tabia nchi | Sh. 450,000,000 |
| **Jumla ya Kifungu** | | **Sh. 624,076,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

**KIFUNGU P02 USIMAMIZI WA MASUALA YA WATU WENYE ULEMAVU**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu S01 | Usimamizi wa Watu wenye Masuala ya Ulemavu | Sh. 155,460,000 |
| **Jumla ya Kifungu** | | Sh. **155,460,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

**KIGUNGU P03 MIPANGO NA UTAWALA**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu S01 | Uongozi na Utawala | Sh. 2,051,997,000 |
| Kifungu S02 | Mipango Sera na Utafiti | Sh. 93,719,000 |
| Kifungu S03 | Uratibu wa Masuala ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba | Sh. 448,148,000 |
| **Jumla Kuu** | | **Sh. 3,373,400,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU B 02 TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UTHIBITI WA MADAWA YA KULEVYA**

**KIFUNGU - P01PROGRAM UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu S01 | Udhibiti wa Usafirishaji na Usambazaji wa Dawa za Kulevya | Sh. 57,814,000 |
| Kifungu S02 | Kinga ya Misingi na Mahitaji na Matumizi ya Dawa za kulevya | Sh. 33,250,000 |
| **Jumla Kuu** | | **Sh. 91,640,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

**KIFUNGU P02 UTAWALA NA UENDESHAJI WA TUME YA DAWA ZA KULEVYA**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu S01 | Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Dawa za Kulevya | Sh.376,036,000 |
| **Jumla Kuu** | | Sh.**467,100,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

**FUNGU B03 - TUME YA UKIMWI**

**KIFUNGU P01 KURATIBU MUITIKO WA TAIFA WA UKIMWI**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu S02 | Mawasiliano na utetezi wa masuala ya ukimwi | Sh.1,034,381,000 |
| Kifungu S03 | Uratibu wa Mitiko ya Kitaifa ya Ukimwi | Sh. 100,833,000 |
| Kifungu S01 | Utumishi na Uendeshaji wa Tume ya Ukimwi | Sh. 383,386,000 |
| Kifungu S02 | Uratibu wa Masuala ya Ukimwi Pemba | Sh. 184,900,000 |
| **Jumla Kuu** | | **Sh.1,703,500,000** |

*(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)*

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya

Fedha ya Ofisi yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makadirio hayo.

Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ameshatoa hoja, wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubaliana na hoja wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri katika Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa kupitisha bajeti yake bila hata ya buti moja ndio maana tunasema wanawake wanaweza ametuthibitishia Mhe. Waziri.

Jengine Waheshimiwa niseme tu kwamba kwa muda uliobakia leo na kwa sababu tumepata vitabu sasa hivi vya Mhe. Waziri, basi ningemuomba Waziri Katika Afisi ya Makamu wa Pili au tumalize, lakini ningeomba Waheshimiwa wajumbe tukisome kitabu kesho tuweze kuchangia vizuri katika Wizara hii.

Baada ya kusema hayo machache sasa naahirisha kikao hadi kesho Saa. 3.00 Asubuhi.

*(Saa 11.58 jioni Baraza liliahirishwa mpaka*
*tarehe 26/5/2015 Saa 3.00 asubuhi)*